# Nipashe

Jumatatu Mei 9, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580940

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710

LIKE & FOLLOW US









**Rais** Mwinyi atangaza nyongeza ya mishahara

UKURASA 5



## KLOPP AANZA KUUKATIA TAMAA UBINGWA EPL

UKURASA 21

# Ndugai aamua kujiweka kando

UKURASA 2



Spika mstaafu, Job Ndugai. **PICHA: MAKTABA**

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**MGOGORO WA KKKT WAENDELEA KUFUKUTA**

MGOGORO wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, umeanza kufukuta...

UKURASA WA 4

**SAMIA ATAJA GHARAMA KUANDAA ROYAL TOUR**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema zaidi ya Sh. bilioni 12.7 zilikusanywa kwa ajili ya...

UKURASA WA 4

**KIKOSI KAZI MAONI YA SIASA CHABADILI RATIBA**

KIKOSI Kazi cha kukusanya maoni ya wadau wa vyama vya siasa na demokrasia kimebadili...


## CHADEMA yabainisha mafanikio ya 'Join the Chain'

UKURASA 3



## Wamiliki wa maduka ya fedha Arusha wamwangukia Samia

UKURASA 3


MICHEZO | MINZIRO AIOTA 3 - BORA GEITA GOLD UK.20 | MAONI, KATUNI UK.6



Mkuu wa Wilaya ya Ileje mkoani Songwe, Anna Gidaya, akizungumza na viongozi wa serikali za vijiji katika mkatno wa wananchi jana, kuhusu uwajibikaji kazini. **PICHA: RAHIM YUNUS**

# Job Ndugai ajiweka kando kwenye ulingo wa siasa

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

SPIKA wa Bunge mstaafu Job Ndugai, ametangaza rasmi nia yake ya kuachana kabisa na siasa.

Amesema hatagombea tena ubunge katika Jimbo la Kongwa mkoani Dodoma.

Ndugai, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza kwenye ibada ya kuweka wakfu gari ya Pareshii ya Mtakatifu Michael Kanisa la Aglikana Tanzania Dayosisi ya Mpwapwa.

"2025 sitagombea nafasi ya ubunge tena nastaafu siyo kama nastaafu kwa kushindwa, lakini ni jambo ambalo tayari nilishalipanga kutoka muda mrefu uliopita hivyo tutaendelea kushirikiana kama ambavyo tunashirikiana sasa,"alisisitiza Ndudai.

Kuacha kugombea tena ubunge ni uamuzi wa pili, baada ya kujiuzulu uspika hivi karibuni na nafasi yake kuchukuliwa na Tulia Ackson.

Ndugai ameliongoza jimbo hilo kwa takribani miaka 20 na kufanikiwa kushika nafasi mbalimbali ikiwamo uenyekiti wa bunge, naibu spika na Spika nafasi ambayo alikuwa nayo hadi anajiuzulu Januari 6, mwaka huu.

Sakata la kujiuzulu kwa Ndugai lilianza mapema mwaka huu baada ya mwishoni mwa mwaka jana kusambaa kwa sauti yake kwenye mitandao ya kijamii akipinga serikali kuendelea kukopa.

Katika sauti hiyo iliyosambaa kwenye mitandao ya kijamii alisikika akisema kuwa nchi kama itaendelea na mikopo ipo siku itauzwa kutokana na madeni.

Baada ya kujiuzulu kwake bunge lilianza mchakato wa kumtafuta Spika mwingine atakaye chukua nafasi yake ambapo uchaguzi ulifanyika Februari mwaka huu na kumchagua Dk. Tulia Ackson kushika nafasi hiyo na Mussa Azzan Zungu kuwa Naibu Spika.

Akizungumzia kuhusu gari hiyo iliyonunuliwa kwa kuchangisha michango kwa waumini wa kanisa hilo pamoja na watu mbalimbali alisema anapongeza wote ambao wamehusika kupatikana kwa gari hiyo.

"Tunapaswa kufanya vitu vyetu wenyewe bila kutegemea mtu aje kutusaidia kwani hata maandiko yanasema kuwa tutakula kwa jasho lakini siyo kwa dezo kama yapo maandiko hayo basi inabidi viongozi wa dini waanze kutufundisha, lakini mimi sijawahi kuyaona," alisema.

Aidha, alisema Watanzania wanapaswa kuondokana na habari ya kutegemea mtu kuja kuwafanyia mambo yao.

Askofu wa Kanisa Aglikana Tanzania Dayosisi ya Mpwapwa, Jacob Chimeledya, alisema ni aibu kuendelea kutegemea wahisani katika kila jambo.

"Ni aibu sisi Watanzania tulivyo na rasilimali za kutosha kuendelea kusubiria wahisani kutoka nje kufanyia mambo yetu ni aibu pia kiongozi wa serikali kuitangaza Tanzania kuwa ni masikini licha ya uwepo rasilimali za kutosha," alisema Askofu Chimeledya.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Antony Mtaka, aliwapongeza waliofanikisha kupatikana kwa gari hiyo ambayo itatumika na kanisa hilo kutatua changamoto za usafiri kila linapo hitajika.

Mtaka, alisema jambo ambalo limefanywa na waumini hao kununua gari bila kusubiri msaada ni jambo la kuigwa na watu wote.

"Lazima sisi kama waumini tuache kitu ambacho tutaendelea kukumbukwa na kanisa na kuwapa wepesi viongozi wa dini katika mahubiri yetu siyo kutunga uongoo kwenye maziko yetu," alisema.

Aidha, aliwataka viongozi wa dini kutumia nyumba zao za ibada kuelimisha masuala mbalimbali ya kijamii ikiwamo zoezi la sensa ya watu na makazi Agosti 23, mwaka huu.

"Tanawashukuru viongozi wa dini kwa kutupa ushirikiano katika mambo mbalimbali ikiwamo wakati wa chanjo ya UVIKO-19 na sasa tunapokwenda kwenye sensa tunaomba ushirikiano wenu wa kutosha kufanikisha zoezi hili," alisema Mtaka.

## Mgogoro KKKT Dayosisi ya Konde bado wafukuta

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOGORO wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Konde, umeanza kufukuta upya baada ya aliyekuwa Askofu wa Dayosisi hiyo, Dk. Edward Mwaikali, kutangaza kuwa yeye bado ni askofu wa dayosisi hiyo, huku akiwataka waumini kuendelea kumuunga mkono ili ashinde vita inayoendelea.

Aidha, baadhi ya waumini wa kanisa hilo ambao ni wafuasi wake wametangaza msimamo mkali wa kumuunga mkono, huku wakituma waraka maalumu kwa Mkuu wa Kanisa hilo, Dk. Fredrick Shoo, ambaye ndiye aliyeongoza mkutano wa kumng'oa madarakani Dk. Mwaikali.

Akizungumza na waumini wa kanisa hilo Jimbo la Kusini katika Usharika wa Makwale wilayani Kyela, Dk. Mwaikali alisema anafanyiwa vurugu kutokana na misimamo yake ya kusimamia mali za kanisa pamoja na ubaguzi wa kikanda.

Aliwataka waumini wa usharika huo kuendelea kumuunga mkono kama ilivyo kwenye maeneo mengine ya dayosisi hiyo ambayo anapata uungwaji mkono kwa kiasi kikubwa tofauti na inavyotangazwa na maadui zake.

"Nilipoona umati huu nimefarijika sana na naamini nitalala usingizi mzuri sana, watu wa Mbeya mpaka sasa wanasema mimi ndiye askofu wao na hawatambui mwingine, sasa ninyi watu wa Jimbo la Kusini nawaomba tushikamane ili tushinde tatizo hili," alisema Dk. Mwaikali.

Vijana wa kanisa hilo wa Jimbo la Mbeya Magharibi wameandaa waraka maalumu ambao wameuelekeza kwa Askofu Dk. Shoo wakimtaka aanze upya kusuluhisha mgogoro huo kabla ya kuendelea na mchakato wa kumweka kazini askofu mpya wa dayosisi hiyo, Geofrey Mwakihaba, ambaye wanadai hawamtambui.

Mwenyekiti wa Idara ya Vijana wa KKKT Jimbo la Mbeya Magharibi, Emmanuel Kaphace, alisema kwa mujibu wa Katiba ya KKKT Dayosisi ya Konde mkutano Mkuu uliofanyika Machi 22, mwaka huu, ulikuwa ni batili.

Alisema hata uchaguzi uliofanyika wa kumchagua Askofu Mwakihaba ni batili hivyo wao bado wanamtambua Askofu Mwaikali kuwa ndiye kiongozi mkuu wa dayosisi hiyo na hawautambui mchakato wowote uliotumika kumuondoa.

Alisema Idara ya vijana ya dayosisi hiyo inamtaka Askofu Dk. Shoo kurejea katika Dayosisi hiyo kwenda kusuluhisha pande mbili zinazovutana akisema awali kiongozi huyo alisikiliza upande mmoja kabla ya kufanya uamuzi.

Kaphace alisema kwa mujibu wa Katiba ya KKKT, uchaguzi wa Askofu unatakiwa kuandaliwa na Halmashauri Kuu ya Dayosisi na siyo Mkuu wa Kanisa kama ambavyo Dk. Shoo alifanya kwenye uchaguzi wa kumchagua Askofu Mwakihaba.

Alisema katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika mwaka 2017, Mwakihaba alikuwa miongoni mwa wagombea waliokuwa wanashindana na Askofu Mwaikali na alishindwa kwa kura, lakini baadaye akachaguliwa kuwa msaidizi wa askofu.

Alisema wakati wa mchakato wa kuhamisha makao Makuu ya Dayosisi kutoka Tukuyu Mjini kwenda jijini Mbeya, Mwakihaba alishiriki lakini baadaye akajiuzulu lakini kwenye uchaguzi wa ulioitishwa na Askofu Shoo wakamchagua kuwa Askofu wa Dayosisi hiyo kinyume na utaratibu.

Akisoma taarifa ya wachungaji hao, Mchungaji wa Usharika wa Mbalizi, Uswege Mwamasinga, alisema kiini cha mgogoro wa dayosisi hiyo ni ubadhirifu uliokuwa umefanywa na baadhi ya waliokuwa viongozi wa kanisa hilo.

Alisema viongozi hao walikuwa wamekopa fedha benki kwa ajili ya upanuzi wa Chuo Kikuu cha Tumaini Mbeya, lakini fedha hizo zikapotea katika mazingira ya kutatanisha na kwamba wanaompinga Dk. Mwaikali wanataka kuuza baadhi ya mali za Kanisa hilo ili kulipa deni hilo.

"Askofu Dk. Mwaikali pamoja na wachungaji tumesimama kwa umoja wetu, hakuna mali ya kanisa itakayouzwa kulipa deni hilo, wachungaji tulitegemea Askofu Shoo angewakutanisha wachungaji wote wa Dayosisi ya Konde kwa ajili ya upatanisho," alisema Mwamasinga.

Alisema kwa mujibu wa Katiba ya Dayosisi ya Konde Toleo la Mwaka 2006, Askofu Mwaikali bado ni Askofu wa Dayosisi ya Konde na kwamba uchaguzi uliofanyika ni batili na hata sherehe za kumuweka wakfu Askofu Mwakihaba ni batili.

Msimamo huo wa wafuasi wa Mwaikali umekuja zikiwa zimebaki wiki chache kabla ya Askofu Mteule Mwakihaba kuwekwa wakfu na kuingizwa kazini ambapo ibada maalumu ya shughuli hiyo inatarajiwa kufanyika Juni 5, mwaka huu, wilayani Rungwe.

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Wilaya ya Sengerema mkoani Mwanza, jana.
**PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Wamiliki maduka ya fedha Arusha wamwangukia Samia

**Cynthia Mwilolezi na Romana Mallya**

WAFANYABIASHARA wa maduka ya kubadilisha fedha jijini Arusha, wanaiomba serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, kuingilia kati ili warudishiwe mali zao na kuwajengea mazingira rafiki, ili waendelee na shughuli hiyo bila vikwazo.

Maombi ya wafanyabiashara hao kwa mkuu wa nchi ni pamoja na kuwarudishiwa fedha, leseni na mali zao zilizochukuliwa wakati wa kufungwa kwa maduka yao na mamlaka za serikali Novemba, mwaka 2018.

Hata hivyo, wameishukuru serikali kwa kuwarudishia simu zao za kiganjani na hati za kusafiria zilizokuwa zimechukuliwa tangu wakati huo.

Akizungumza na Nipashe, mmoja wa viongozi wa wafanyabiashara hao, Melance Kisoka, alisema baada ya Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, kulieleza Bunge kuwa walisharudishiwa vitu vyao, lakini walichorudishiwa ni simu na hati za kusafiria pekee.

"Kwa kweli leseni zetu na fedha zetu, mali zingine kama nyumba na magari hazijarudishwa kwetu na hatujui sababu," alisema.

Alisema pia hata serikali ikiwarudishia fedha zao kwa sasa wengi wao watashindwa kuendelea na biashara hiyo kwa sababu ya ongezeko la mtaji wa kuanza biashara hiyo kuongezwa kutoka Sh. milioni 300 hadi Sh. bilioni moja.

Kisoka alisema mwaka 2015 mtaji kwa mtu aliyetaka kuingia biashara hiyo ulikuwa usipungue Sh. milioni 40 na baada ya hapo ikapanda hadi Sh. milioni 100 ambayo ilikuwa mwisho wa kuilipa mwaka 2017.

"Sasa kabla hata ya tarehe ya mwisho iliyopangwa tuwe umelipa mwaka huo ukapandishwa hadi Sh. milioni 300 na wakati tumeanza kulipa hapo katikati tukavamiwa kwenye maduka yetu na kunyang'anywa, fedha, simu, hati za kusafiria na leseni, huku baadhi wakichukuliwa magari na nyumba zao nangari leo serikali haijarudisha,"alisema.

Alisema wanaiomba serikali iwarudishie mali zao hizo ili waendelee na maisha mengine.

Hata hivyo, alisema maridhiano juu ya usalama wa kuanzisha upya maduka hayo ni muhimu, kwa kuwa ni muhimu kuhakikishiwa usalama wa biashara zao ili yasijirudie yaliyojitokeza mwaka 2018.

"Hapa tunaomba tuhakikishiwe usalama na juu ya kuheshimu sheria za uanzishwaji wa maduka haya kama hawatatuvamia tena ili turejeshe imani kwa serikali," alisema. Naibu Waziri Masauni, alisema bungeni kuwa wafanyabiashara hao warudishiwe vitu vyao ili wafungue maduka hayo, lakini hadi sasa wengi wameshindwa kufungua.

**SERIKALI WARUSHIANA 'MPIRA'**

Mkurugenzi wa Huduma na Elimu kwa Mlipa Kodi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Richard Kayombo, alipotafutwa na Nipashe Alhamisi iliyopita alisema hana mamlaka ya kuzungumzia suala hilo na kutaka itafutwe Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa sababu ndiyo inayohusika na maduka ya fedha. Meneja Msaidizi Idara ya Uhusiano wa Umma kutoka BoT, Vick Msina, alipotafutwa kujua nini kinaendelea kuhusiana na fedha na mali za wafanyabiashara hao alisema kuwa aliyeongoza operesheni hiyo ni DPP (Mkurugenzi wa Mashtaka) hivyo aulizwe yeye.

Gazeti hili lilipomtafuta DPP, Sylvester Mwakitalu, alisema hafahamu chochote mpaka afuatilie kujua majalada hayo yakoje.

"Labda nifuatilie sina taarifa yawezekana majalada yapo lakini sijapata kuyaona," DPP Mwakitalu aliomba.

## CHADEMA yafunguka mafanikio 'Join the Chain'

**Na Maulid Mmbaga**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Benson Kigaila, amesema programu yao ya (Join the Chain) imekisaidia chama kujitegemea kimapato na kujiendesha bila kupokea ruzuku kutoka serikalini.

Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, amekuwa akionekana mara kadhaa akizunguka katika maeneo mbalimbali nchini akichangisha na kupokea michango kutoka kwa wanachama wa CHADEMA huku akieleza kuwa chama hicho kitaendeshwa na wananchi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kigaila alisema programu hiyo ina malengo makuu mawili ikiwamo kuwafanya Watanzania waungane katika suala la kudai katiba mpya na kukitegemeza chama kimapato, jambo ambalo alidai kuwa limefanikiwa kwa kiasi kikubwa.

"Taasisi sustainable (endelevu) lazima iwe na uwezo wa kupata mapato kutoka ndani yake bila kutegemea wafadhili au hisani ya serikali, na imefanikiwa ndiyo maana CHADEMA leo ipo haichukui ruzuku, lakini inafanya shuhuli zake zote kama kawaida," alisema na kuongeza:

"Kila programu imefanikiwa sana, na sisi CHADEMA hatujawahi kubuni progamu, ikashindwa kwasababu tunabuni kwa ajili ya watu." Aidha, alibainisha kuwa baraza kuu la chama hicho linatarajia kukaa Mei 11, mwaka huu, na ajenda mojawapo zitakazo jadiliwa itakuwa ni rufani ya wabunge wa viti maalumu wa chama hicho Halima Mdee na wenzake 18 na kufanya uamuzi.

Alisema baraza hilo linakutana kwa mujibu wa katiba kwa ajili ya kujadili ajenda zake huku alidai kuwa endapo kutakuwa na rufani yoyote imeletwa kwake litatumia muda huo kujadili ajenda hiyo ya rufani. Vilevile, alitoa wito kwa wanachama wa chama hicho na Watanzania kwa ujumla kuungana katika kudai katiba mpya, ili iweze kuwafungulia ukurasa mpya ambao utaifanya nchi iendeshwe kwa mujibu wa katiba na sheria na siyo kwa tamko la mtu mmoja kwa sababu ya chuki chake.

Hivi karibuni Mbowe, alikaririwa akisema kuwa chama hicho kitajiendesha kwa kutegemea fedha za Watanzania na hawatarajii kuomba au kupokea ruzuku ya serikali.

Aidha, tangu alipoachiwa Machi 4, mwaka huu, kampeni ya Join the chain ilishaanza, na alipotoka alionekana kwenye maeneo ya Tegeta, Kunduchi na Kariakoo mkoani Dar es Salaam akiendeleza kampeni hiyo huku wananchi wakijitokeza kutoa fedha.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO Mkoa DODOMA**
**Usimamizi wa mirathi Na 25/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU HAMISI HAMADI BWASHE WA VEYULA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ASHA ALLY HAJI**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 11 Mwezi 05 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
**Imtolewa leo tarehe 05/05/2022.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 63 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DORICE DANIEL MBOGONI of Iyumbu within Dodoma City.**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATIONFOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY CURTES JEFFREY MBOGONI**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES Gn. 369Of 1963)**

ALL PERSONS Claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 12-th Day of May, 2022.
Dated at Dodoma this 28th day of April, 2022

RESIDENT MAGISTRATE I/C

**NYUMBA YA MAKAZI INAUZWA-TEGETA UNUNIO MASAITI BEACH**

ENEO ILIPO: TEGETA UNUNIO MASAITI UPANDE WA BEACH-DAR ES SALAAM

NYUMBA YA MATOFALI INA VYUMBA VINNE KIMOJA MASTER, SITTING NA DINNING ROOMS KUBWA, JIKO NA STOO VYOTE VINA MARUMARU (TILES).

INA NYUMBA YA MFANYAKAZI (SERVANT QUARTER) YENYE CHOO, BAFU NA STOO.

INA UZIO WA TOFALI NA GETI LA KUSUKUMA (SLIDING).

ENEO LA KUEGESHA MAGARI MATATU.INA HATI KAMILI

**MAWASILIANO:0673-338658**
**MHINA MOHAMED**

**NAFASI ZA KAZI**

Kampuni ya Madawa iliopo Dar es salaam inahitaji **MEDICAL REPRESENTATIVE.**

Kwa mawasiliano piga simu namba **0713 786300.**

# Samia aanika gharama kutengeneza Royal Tour

**Na Maulid Mmbaga**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amesema zaidi ya Sh. bilioni 12.7 zilikusanywa kwa ajili ya kutengeneza filamu ya Royal Tour huku aliyefanya kazi hiyo akilipwa Sh. bilioni 7.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, wakati wa hitimisho la uzinduzi wa filamu hiyo nchini, alisema walikuwa na malengo ya kukusanya Sh. bilioni 20 lakini walipata ahadi ya Sh bilioni 19.39 ambazo zilichangiwa na sekta za uwekezaji uzalishaji na biashara, sekta ya fedha na utalii.

"Kulikuwa kuna hoja kadhaa kuhusu matumizi ya fedha, nataka nikiri kwenu kwamba fedha yote tuliyokusanya ndiyo iliyotumika kwenye Royal Tour, na tulitumia Sh. bilioni saba kulipa kampuni iliyofanya shooting na kutengeneza filamu nyingine.

"Kuna fedha pia tulitumia kamati kwenda kurudi safari (Marekani) na kila kitu, nataka niwahakikishie Royal Tour hatua ya kwanza ndiyo hii tuliyoiona, lakini walio 'shoot' walichukua picha nyingi hivyo fedha tuliyonayo tunakwenda kuendeleza awamu ya pili na tatu ya Royal Tour na ndege zote za kimataifa zinazokuja hapa tutawapa hizi filamu waweze kuzionesha," alisema Rais Samia.

Aidha, aliwapongeza Watanzania na sekta binafsi kwa kushiriki kikamili katika kuandaa hadi kukamilika kwa filamu hiyo ambayo imeshazinduliwa Marekani, Arusha na Zanzibar.

Rais Samia alisema Mei 3, mwaka 2021 alikutana na wadau wa sekta binafsi na akatangaza adhima ya kuitangaza Tanzania, ilipofika Juni 26, 2021, alifanya kikao cha 12 cha Baraza la Biashara Tanzania kuwaomba kuunga mkono na walikubali.

Kwa mujibu wa rais, uandaaji wake ulikuwa na changamoto kwa upande wake kwa kuwa ilikuwa ni mpya kwake na kugomewa na maofisa wake kushiriki baadhi ya vipengele vya filamu hiyo.

Aidha, alieleza kuwa filamu hiyo itakuwa ni kitu kitakachobaki kama urithi kwa vizazi vya sasa na vijavyo, huku akieleza kuwa itakuwa siyo ya kuangaliwa pekee bali kunufaika na fursa kwa kuwa imefungua njia na kutoa msukumo kwa Watanzania kuitangaza nchi na kuleta wageni.

Kwa mujibu wa Rais Samia, filamu hiyo pia itasaidia sekta ya utalii, huku akibainisha kuwa imeajiri asilimia 4.5 ya Watanzania, na alieleka kuwa utalii wakati wa UVIKO-19 ulishuka kwa asilimia 27 na watu 412,000 walipoteza ajira zao.

"Ili turudi tulikotoka kwa nguvu lazima kuwe na matangazo ya nguvu kuitangaza Tanzania na kilichotusukuma wote tunajua maeneo ya utalii kama Arusha unaona miji imejiinamia, kwa hiyo mbali na mapato ya kitaifa lakini sekta hii inakwenda kwenye pato la mtu mmoja moja kwa moja," alifafanua Rais Samia.

Awali, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Filamu hiyo, Dk. Hassan Abbas, alisema vituo vyote vya televisheni nchini vimepewa ruksa ya kuonyesha filamu ya Royal Tour baada ya hitimisho la uzinduzi huo uliofanyika Dar es Salaam.

Pia, alitoa pongezi kwa wanakamati waliohusika katika mchakato wa kuandaa filamu hiyo pamoja na mtayarishaji, Peter Greenberg kwa kutengeneza kazi nzuri yenye viwango vya Hollywood ambayo imesaidia kuonyesha mandhari na rasilimali mbalimbali za utalii zilizoko nchini.



Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, akikagua ujenzi wa barabara ya Gangilonga inayojengwa kwa kiwango cha lami mjini Iringa juzi. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Kikosi kazi maoni ya siasa chabadili ratiba

**Na Jenifer Gilla**

KIKOSI Kazi cha kukusanya maoni ya wadau wa vyama vya siasa na demokrasia kimebadili ratiba yake iliyotolewa tarehe 5 Mei, 2022.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu wa Kikosi Kazi hicho, Sisty Nyahoza, wajumbe wa Kikosi Kazi wataanza kukutana na taasisi pamoja na watu binafsi badala ya vyama vya siasa kama ilivyoelezwa awali.

Kwa mujibu wa ratiba hiyo, Kikosi Kazi kitaendelea kukutana na wadau mbalimbali wa demokrasia ya vyama vingi nchini kuanzia 10 Mei, 2022 kwenye ukumbi wa Chifu Adam Sapi Mkwawa, ofisi ndogo za Bunge jijini Dar Salaam.

"Siku hiyo Kikosi Kazi kitaanza kwa kukutana na Taasisi ya The Right Way kuanzia saa nne hadi saa tano asubuhi. Mchana kuanzia saa sita kitakutana na Msajili wa Vyama vya Siasa Mstaafu John Tendwa na kukamilisha ratiba yake kwa kukutana na Kituo cha Utawala Bora na Maendeleo (CEGODETA) kuanzia saa nane hadi tisa mchana," alisema Sisty.

Vile vile taarifa huyo ilisema kuwa siku ya Jumatano itakuwa zamu ya Jumuiya ya Wahindu Tanzania kuanzia saa nne hadi tano asubuhi. Mchana Kikosi Kazi kuanzia saa sita mchana kitapata wasaa kupokea maoni ya Sheikh Ponda Issa Ponda na baadaye Askofu Emaus Mwamakula wa Kanisa la Moravian.

Pia Alhamisi Kikosi Kazi saa nne asubuhi kitakuna na Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe Benson Bagonza, mchana kuanzia saa sita itakuwa zamu ya Dk. Hellen Kijo Bisimba kuwasilisha maoni yake na baadaye wa fani ya sheria Prof. Issa Shivji.

Taarifa iliendelea kueleza kuwa siku ya Ijumaa Kikosi Kazi kitapokea maoni ya mwanazuoni wa fani ya sheria na mwanahabari mkongwe Jenerali Twaha Ulimwengu na mwanasheria Fatma Karume kuanzia saa tatu hadi tano asubuhi. Pia taarifa hiyo inaonyesha wiki inayoanza Mei 16, Kikosi Kazi kitaendelea kukutana na taasisi mbalimbali na watu binafsi. Kikosi Kazi kitakutana na taasisi kama Chama cha Wakulima Tanzania (TASO), Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Mtandao wa Wanawake wa Katiba, Uchaguzi na Uongozi Tanzania.

Ilifafanua kuwa watu binafsi ni pamoja na mwanahabari Maria Sarungi, Wadhibiti na Wakaguzi Wakuu wa Hesabu za Serikali wastaafu Profesa Mussa Assad na Ludovick Utouh.

# Wawekezaji wasio na EIA wasakwa

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limewataka wawekezaji walioanza biashara bila kufanya Tathmini ya Athari za Mazingira (EIA), wajisalimishe ili waweze kufanyiwa tathmini na kupewa vyeti kuepuka adhabu.

Tangazo hilo lilitolewa na Meneja wa NEMC Kanda ya Magharibi, Benjamin Dotto, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu maonyesho ya Kimataifa ya Biashara ya nchi zinazozunguka Ziwa Tanganyika yanayoendelea mkoani Kigoma.

Maonyesho hayo yanafanyika katika uwanja wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), uliopo karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kigoma.

Alisema kwa utaratibu wa kisheria wawekezaji wanaoanza kuwekeza bila kuwa na (EIA) wanapaswa kupewa adhabu lakini wakijisalimisha watafanyiwa ukaguzi na kupewa vyeti na kuendelea na shughuli zao kama shughuli zao haziathiri mazingira.

"Ili kuepuka adhabu tunawashauri wajitokeze wenyewe kwenye maonyesho ya Kigoma ambapo watafanyiwa ukaguzi wa awali kuona kama shughuli wanazofanya hazina athari kwa mazingira ili wapewe vyeti waendelee na shughuli zao," alisema.

Alisema NEMC imeshiriki katika maonyesho hayo ili kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira pamoja na usajili wa miradi, ulipaji wa ada na tozo na tathmini ya athari kwa mazingira na mambo mengine mbalimbali. "Maonyesho haya ni muhimu yatasaidia sisi baraza kutoa elimu kuhusu utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa wananchi wanaoshiriki katika maonyesho haya ambayo yanajumuisha nchi zote zinazozunguka Ziwa Tanganyika yaani Tanzania, Rwanda, Burundi, Zambia na Congo DRC," alisema Dotto.

Ofisa Mazingira kutoka NEMC Kanda ya Mashariki, Edith Makungu, aliwataka wananchi washiriki katika maonyesho hayo pamoja na kutilia maanani suala la ulipaji wa ada na tozo za mazingira ambalo mwisho wa malipo hayo ni tarehe 30 Juni mwaka huu.

"Tunawasisitiza na kuwakumbusha wale wote ambao hawajalipa tozo na ada za mazingira kujitahidi kulipa ndani ya muda kwani kulipa ada na tozo za mazingira ni muhimu kwa mustakabali wa maendeleo ya Taifa letu," alisema.




Maandamano ya wafanyakazi kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani yaliofanyika jana, katika viwanja vya Maisara Suleiman na kupokelewa na Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi atangaza nyongeza ya mishahara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametangaza kuongeza kiwango cha mishahara kwa watumishi wa umma kuanzia Julai mwaka huu, katika mwaka wa fedha wa 2022/2023.

Alitangaza kuongeza kiwango cha mishahara akiwahutubia wananchi katika kilele cha sherehe za Siku ya Wafanyakazi Duniani, iliyoadhimishwa jana katika viwanja vya Maisara Mjini Zanzibar.

Alisema kuwa ongezeko hilo la mishahara litazingatia kiwango cha elimu na uzoefu wa kazi kwa watumishi wa umma, na kwamba ongezeko hilo litakua na mchango wa kuimarisha uwezo wa utumishi wa umma, ili kuendanana na mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na hali ya maisha katika uhalisia wake.

Alisema serikali imetenga jumla ya Sh. bilioni 12.7 kwa mwezi sawa na Sh. bilioni 153 kwa jili ya kugharamia utekelezaji wa zoezi hilo la ongezeko la mishahara.

Alieleza kuwa kiwango cha chini cha mshahara kwa mtumishi mpya utapanda kutoka Sh. 300,000 hadi kufikia Sh. 347,000 ikiwa na ongezeko la asilimia 15.6.

Alisema kwa mtumishi wa elimu ya ngazi ya cheti kwa masomo ya sanaa, mshahara wake utapanda kutoka Sh.321,000 hadi kufikia Sh. 382,000 ikiwa ni ongezeko la asilimia 19.

"Hapa tunakusudia kwamba kila mfanyakazi atapata nyongeza ya mshahara kutokana na elimu yake na muda aliofanya kazi hapo nyuma tulizoea kusikia tumepandisha kima cha chini wote huwa fungu moja, lakini leo yule ambaye yupo kazini kwa muda wa miaka 10 hatakuwa sawa na mfanyakazi mpya," alisema.

Alisema serikali itaendelea kuhakikisha wafanyakazi wanaendelea kupata haki zao kwa wakati na kuendelea kuimarisha mazingira ya ufanyaji kazi, ili kufanya kazi katika mazingira mazuri.

Rais Mwinyi alisema kwa lengo la kuimarisha misingi ya utawala kwenye utumishi serikali ipo katika hatua za mwisho ya kufanya marekebisho ya mkataba wa ajira katika utumishi wa umma, ambao unapaswa kuajiriwa na kila mtumishi wa umma anapoanza kazi.

"Marekebisho haya yamelenga kufafanua kwa uwazi zaidi wajibu wa utumishi wa umma pamoja na kuimarisha haki na maslahi yake katika kipindi chote cha utumishi wake," alisema.

Aidha, alisema katika kuhakikisha wafanyakazi wanaendelea kuwa na kipato hata wanapata changamoto ya kupoteza ajira au wakupata ajali wakiwa kazini serikali kupitia mfuko wa hifadhi ya jamii Zanzibar imeazisha fao la upotevu wa ajira na fao la kuumia kazini ambayo yataanza kutolewa mwaka ujao wa fedha.

"Nawaahidi watumishi wa umma kwamba serikali itaendelea kuimarisha maslahi ya umma kadri hali ya uchumi itakaporuhusu,"alisema.

Hata hivyo, alisema kuwa serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya wapya 5,936 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, katika sekta mbalimbali za utumishi wa umma na imeshatenga Sh. bilioni 24.6 katika bajeti ya mwaka 2022/2023 kwa ajili ya kugharamia ajira hizo.

Dk. Mwinyi alisema kuwa bado kuna tatizo kubwa la kukokosekana kwa utaalamu na ujuzi wa kutosha katika utumishi wa umma, hali inayopelekea kuwepo kwa ufanisi mdogo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kazi mbalimbali katika taasisi.

Akisoma risala ya wafanyakazi, Katibu wa Chama cha Wafanyakazi Zanzibar, Khamis Mwinyi, alisema kuwa bado kuna baadhi ya wafanyakazi ambao walikuwamo katika mfumo wa ugatuzi bado hawajapata haki zao.

Alisema kuna changamoto ya wafanyakazi ambao wameitumikia serikali chini ya miaka 10 hawajapewa pensheni yao baada ya kustaafu jambo ambalo ni dhuluma kubwa.

"Kuna wafanyakazi ambao wametuhumiwa kwa muda mrefu wapo nje hawachukuliwi hatua, hawapewi chochote na wengine wanafikia karibu ya kustaafu. Tunakuomba Rais yashughulikiwe masuala haya maana yanasikitisha sana,"alisema.

Alisema kuwa viongozi anaowateuwa hawashughulikii masuala hayo na baadhi wamekuwa na jeuri na kiburi wanapopeleka malalamiko ya wafanyakazi hawataki kuwasikiliza.

Akizungumzia kuhusu vikokotoo, alisema ni mtihani mkubwa kwa sababu pensheni imepunguza kwa asilimia 40 katika mfuko wa hifadhi ya jamii, jambo ambalo ni kilio kikubwa hivyo alitaka serikali kuendelea kulifanyia kazi suala hilo kwa sababu watu wanaendelea kuumia.

Kwa upande wake Mwakilishi wa Shirika la Kazi Duniani (ILO), Kanda ya Afrika ya Mashariki, Wellington Chinese, aliipongeza serikali ya Zanzibar kukabiliana na tatizo la ajira za watoto na kuwarejesha shule watoto walioingiza katika ajira hizo ili kuwa na vijana wasomi.

Aidha, alipongeza juhuzi za serikali kujenga mazingira mazuri, ikiwamo kazi za staha na marekebisho ya sheria lengo kuleta ufanisi wa kazi.

Zanzibar imeadhimisha Siku ya Wafanyakazi jana Mei 8 kwa sababu ya kuwapa nafasi wafanyakazi kufanya maandalizi ya sikukuu ya Iddi ambapo Mei Mosi, ilikuwa ni sawa na Ramadhani ya 29, na kauli mbiu ya maadhimisho hayo ni kutimiza wajibu kazini, na kupata haki kwa wafanyakazi ni nguzo ya utawala bora.

# DC Basila Mwanukuzi apata ajali, alazwa

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Korogwe, Basila Mwanukuzi amelazwa katika Hospitali ya Rufani Mkoa wa Tanga baada ya kupata ajali juzi katika eneo na Hale, barabara ya Tanga-Segera.

Hata hivyo imeelezwa kuwa hali yake inaendelea vizuri.

Kaimu Kamanda Polisi Mkoa wa Tanga, David Mwasimbo, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo huku akisema kuwa chanzo ni mwendokasi, majeruhi wakiwa wanne, akiwamo DC ambaye amevunjika mguu.

"Ajali imetokea usiku wa kuamkia leo (jana), Mkuu wa Wilaya anaendelea vizuri isipokuwa dereva wake hali si nzuri, chanzo cha ajali ni mwendokasi. Dereva alikuwa anajaribu kuyapita magari mengine na ndipo ajali ikatokea," alisema.

Mganga Mkuu wa Hospitali ya Rufani ya Bombo, Dk. Jonathan Gudemo, alisema aliwapokea majeruhi watatu wa ajali hiyo wawili kati yao ikiwamo DC Mwanukuzi wanaendelea vizuri.

"Majeruhi wawili hali zao zinaendelea kuimarika ikiwamo DC Mwanukuzi, huku majeruhi mmoja yupo chini ya uangalizi wa matibabu na mmoja tumempatia rufani ya kwenda Muhimbili kwa ajili ya matibabu zaidi," alisema.

# Mitihani kidato cha sita, ualimu kuanza leo

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA) limetangaza kuanzia leo mitihani ya kidato cha sita na ya ualimu inatarajia kuanza na itafanyika kwa siku 19, huku idadi ya watahiniwa wanawake waliosajiliwa ikionyesha kuwa ndogo ikilinganisha na wanaume.

Katika mtihani wa kidato cha sita jumla ya watahiniwa 95,955 wamesajiliwa kuufanya ambapo wa shule ni 85,531 na kati yao wanaume ni 47,859 sawa na asilimia 55.96 na wanawake ni 37,672 sawa na asilimia 44.04.

Kati ya watahiniwa wa kujitegemea 10,424 waliosajiliwa, wanaume ni 6,546 sawa na asilimia 62.80 na wanawake ni 3,878 sawa na asilimia 37.20.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, aliyasema hayo jana mkoani Dar es Salaam na kueleza kuwa mitihani hiyo itafanyika kuanzia leo hadi Mei 27, mwaka huu.

"Mitihani hii itafanyika katika jumla ya shule za sekondari 841, vituo vya watahiniwa wa kujitegemea 250 na vya ualimu vitakuwa ni 70 Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar," Msonde alisema.

Alisema watahiniwa wenye mahitaji maalum wapo 151 na kati yao, 136 ni wenye uoni hafifu na 15 ni wasioona ambapo mmoja (asiyeona) ni mtahiniwa wa kujitegemea.

Kwa upande wa mtihani wa ualimu, Dk. Msonde alisema jumla ya watahiniwa 9,670 wamesajiliwa kufanya na kati yao, 4,560 ni ngazi ya Stashahada na 5,110 ni ngazi ya cheti.

Alisema kati ya watahiniwa 4,560 wa ngazi ya stashahada waliosajiliwa, 2,960 sawa na asilimia 64.91 ni wanaume na 1,600 sawa na asilimia 35.09 ni wanawake.

"Kati ya watahiniwa 5,110 wa ngazi ya cheti waliosajiliwa, 2,336 sawa na asilimia 45.71 ni wanaume na 2,774 sawa na asilimia 54.29 ni wanawake. Watahiniwa wenye uoni hafifu wapo wawili na wasioona ni wawili," alisema.

Alisema kutokana na umuhimu wa mitihani hiyo, baraza linazitaka Kamati za Mikoa na Halmashauri, Manispaa, Jiji kuhakikisha taratibu zote za uendeshaji mitihani ya Taifa zinazingatiwa ikiwamo kuwapo kwa mazingira salama, tulivu na kuzuia mianya ya udanganyifu.

Pia, baraza limewataka wasimamizi wote kufanya kazi zao kwa umakini na uadilifu na kwa watahiniwa wenye mahitaji maalum waongezewe muda wa dakika 20 kwa kila saa kwa somo la Hisabati na dakika 10 kwa kila saa kwa masomo mengine.

Dk. Msonde alisema baraza linawaasa wasimamizi wa mitihani, wamiliki wa shule, walimu na wananchi wote kwa ujumla kutojihusisha na vitendo vyovyote vya udanganyifu wa mitihani huo kwani halitasita kuchukua hatua.

Pia aliwaomba wadau wote kutoa taarifa katika vyombo husika kila wanapobaini mtu au kikundi cha watu kinajihusisha na udanganyifu wowote.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mijadala ya kuinua soka ifanyiwe kazi, tusifungiane

**SOKA** letu linahitaji uwanja huru na mpana zaidi katika kujadili maendeleo yake na vikwanzo vinavyochangia kushindwa kusonga mbele kwa kasi zaidi kutoka hapa tulipo na kufikia nchi zilizopiga hatua Afrika kama vile Morocco, Misri, Algeria, Tunisia, Afrika Kusini na nyinginezo nyingi zilizopo juu yetu.

Kubaki kusema tu kwamba ligi yetu ni miongoni mwa ligi 10 bora barani Afrika, hakutasaidia kitu hasa kutokana na ukweli kwamba bado klabu zetu hazifanyi vizuri kwenye michuano inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Hii ni kutokana na misimu miwili mfululizo ambayo tumeingiza timu nne kwenye michuano hiyo ya CAF; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho Afrika, bado tumekuwa tukibaki na timu moja tu, Simba ambayo imekuwa ikiishia robo fainali.

Takwimu ndizo zinazoweza kuwafanya Watanzania kila mmoja kutembea kifua mbele kwamba ligi yetu ni bora, kwa kumulika namna klabu zetu zinavyofanya vizuri kwenye michuano hiyo ya Afrika na si vinginevyo.

Na kwa kuanika vigezo na takwimu kama hizo, ni wazi kutaongeza ari ya wachezaji kupambana kuweza kufika mbali kwenye michuano hiyo ya Afrika ambayo inaongoza kwa utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani humu.

Tumelazimika kulimulika hilo kutokana na woga mkubwa kwa wenye uwezo wa kulisemea, wakiogopa kwamba wanaweza kufungiwa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), kwa kale kawoga kwa 'mwanafamilia wa soka' kulikosoa soka letu.

Tumeona mwishoni mwa wiki namna ambavyo hoja nzuri iliyotolewa na Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally ambaye yeye kama mdau wa soka, alidai kuwa timu zinazocheza Ligi Kuu msimu huu zimekuwa dhaifu kwa sababu nyingi zinapigania kuepuka kushuka daraja.

Lakini kutokana na itikadi za Watanzania kubebwa na Usimba na Uyanga, upande wa pili wamekuwa wakigeuza maneno kwa kueleza kwamba alisema "ligi yetu" ni dhaifu, jambo ambalo kwetu sisi tunaona hata kama Ahmed angekuwa amesema hivyo bado si dhambi kwa hoja alizozitoa.

Kinachoonekana ni baadhi kujitokeza kupindua maneno, wakitaka kuona TFF ikimchukulia Ahmed hatua, kitu ambacho sisi tunaona kwa shirikisho hilo kuthubutu kufanya hivyo, kutazidi kuwafanya wadau wa soka wenye nia njema ya kutoa hoja zao za msingi katika kulijenga soka letu kufunga midomo yao.

Kwa kuwafunga mdomo wadau wa soka wenye weledi mkubwa, ni wazi Tanzania itaendelea kuchechemea hapo ilipo kwa miaka mingi zaidi kwani mpira wetu unahitaji uwazi na ushirikishwaji wa maoni kwa kila mwenye nia njema nao.


Hoja aliyoitoa Ahmed akielezea kwamba timu nyingi ni dhaifu hasa akitolea mfano kuwa kati ya timu 16 zinazoshiriki ligi hiyo msimu huu, ukitoa Simba na Yanga, zilizobaki zote zinapigania kuepuka kushuka daraja na si ubingwa, ni jambo la kutazamwa na kufanyiwa kazi na si kutaka kumfanya kuonekana msaliti.

Tunahitaji kuona akipingwa kwa takwimu, na si baadhi ya wadau wa soka kumlisha maneno wakieleza kwamba alisema ligi ni dhaifu na kwa kufanya hivyo eti anawakatisha tamaa wadhamini ambao wamewekeza kiasi kikubwa cha fedha.

Tunaamini mdhamini yeyote anahitaji kuweka fedha kwenye ushindani mkubwa ili kupata 'walaji' wa bidhaa anayoitangaza, hivyo hoja ya Ahmed hata kama angesema ligi yetu ni dhaifu, bado ingepaswa pia kuchukuliwa kama changamoto kuanzia kwa klabu shiriki, viongozi, TFF na Bodi ya Ligi, TPLB.

Nipashe tukiwa kama wadau namba moja wa michezo nchini, pia tunatamani kuona wakati kama huu zaidi ya timu sita zikiwa zina nafasi sawa ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu jambo ambalo lingezidi kuhamasisha wawekezaji kujitokeza kuwekeza na si kama ilivyo sasa timu 14 zikipambana kuepuka kushuka daraja. Hivyo tuache woga na TFF ipokee maoni na kuyafanyia kazi ili msimu ujao kuwe na ushindani mkubwa wa ubingwa na si wa kuepuka kushuka daraja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Timu zingekuwa bora, Simba ya sita

**MJADALA** umeendelea kuwa mkali sana kwenye vituo vya redio, televisheni, mitaani, hasa kwenye vijiwe vya kunywa kahawa, mipira, vituo vya wauza magazeti, mabasi, ndani ya daladala na kwenye mitandao ya kijamii ndiyo balaa.

Ni ule ulioanzishwa na Meneja Habari na Mawasiliano, Ahmed Ally ambaye yeye kama mdau wa soka, alidai kuwa timu zinazocheza Ligi Kuu msimu huu zimekuwa dhaifu kwa sababu nyingi zinapigana ili zisishuke daraja.

Akasema kati ya 16 zinazocheza Ligi Kuu, ni timu mbili tu za Simba na Yanga ndizo haziwezi kushuka, lakini zilizobaki zote 13 kama hazikuchanga karata sawasawa zinaweza kushuka.

Ahmed aliongea kitakwimu zaidi. Na ni kweli, kwani timu ya mwisho hadi ya tatu kuna tofauti ya pointi 11 tu. Timu zimeachana pointi chache sana. Msimu huu kumeonekana kuwa kila timu na ufalme wake. Yanga inayoongoza ligi imekuwa ikiizidi timu ya pili Simba kwa pointi zisizopungua 10, huku Wekundu wa Msimbazi nao wakiwa kwenye utawala wao, kwani imeizidi Azam FC inayoshika nafasi ya tatu pointi zaidi ya 10. Ila kuanzia ya tatu hadi ya mwisho zenyewe pointi zao zinafuatana.

Akasema ni hatari kuwa na ligi ambayo timu zinashindana kubaki Ligi Kuu na si kushindana kutwaa ubingwa. Hata timu yake akaitaja kuwa ni moja kati ya zilizoonyesha udhafu msimu huu.

Baadhi ya wanamichezo hawakuipokea vizuri kauli hii. Kila mmoja alikuwa na sababu yake na kila mtu alikuwa na hoja yake. Mjadala umeendelea kuwa mkali mno. Jumamosi kwenye safu hii niliandika kuwa, inawezekana Ahmed akawa na hoja, kwani kama kuna timu zinashangilia sare, ujue kuna matatizo.

Nikasema ukitaka kujua timu kwenye Ligi Kuu ni dhaifu, angalia zikicheza na Simba au Yanga, zinakaa nyuma, zinahitaji zaidi sare kuliko ushindi, zikibahatika kupata bao moja, basi ni hilo hilo. Tena zitaanza kupoteza muda.

Ndiyo maana zikipata sare, wachezaji wao wanashangilia na kuzunguka uwanja, unaweza kudhani zimetwaa ubingwa. Timu inayosaka ubingwa haiwezi kushangilia sare dhidi ya Simba au Yanga. Jiulize Simba au Yanga, kufungwa mabao 2-0, 3-0, 3-1, ilikuwa lini?

Miaka ya nyuma, Simba au Yanga kupigwa idadi hiyo ya mabao ilikuwa ni kitu cha kawaida tu, tena ikiwa na wachezaji bora kabisa wanaochezea mpaka timu za taifa ikiwamo wanaoichezea Taifa Stars.

Zinafungwa na hazikamiwi, ila zinachezewa mpira haswa. Hakuna kupaki basi. Na haikuwa mara ya kwanza mbili au tatu kufungwa na timu mbalimbali kwa idadi kubwa ya mabao. Hii ndiyo unaweza kusema ligi bora na timu zilikuwa bora. Kwa hizi timu zinazoshangilia sare, zikicheza kutaka kusalia Ligi Kuu, badala ya kubishana inafaa tuangalie tatizo ni nini?

Naendeleza tena mjadala huu kwa kutoa hoja nyingine. Msimu uliopita, mastraika watatu wa Simba, Meddie Kagere, Chris Mugalu na John Bocco walifunga jumla ya mabao 44. Leo hii mastraika hao wote wana mabao saba tu, na yote amefunga Kagere. Lakini eti bado Simba ipo kwenye nafasi ya pili. Tena kwa zaidi ya pointi 10. Kwa ligi yoyote bora, yenye timu bora, haiwezekani timu iwe na mastraika ambao mpaka timu inaelekea ukingoni hawajafunga hata bao moja, iwe ya pili, ikizipita timu zingine kwa mbali sana.

Mabao ya Simba kwa sasa yanafungwa na viungo tu. Nilitegemea udhaifu, ungetumiwa na timu zingine kuitupa chini kabisa ya msimamo kwenye nafasi ya nne mpaka ya sita.

Inawezekana tatizo linaanzia mbali sana. Huenda nchi kwa sasa haina wachezaji wenye viwango bora kama wale wa zamani, au wachezaji washindani, wapambanaji.

Au aina ya mafunzo wanayoyapata hayakidhi, na labda hawapati mazoezi ya kutosha ya fiziki mwanzoni mwa msimu.

Au huduma za baadhi ya timu kwa wachezaji wao, kama vile mishahara, chakula, posho, usafiri ni duni ukilinganisha na timu zingine, ndiyo maana inakuwa hivyo.

Mfano, Simba na Yanga zinasafiri kwa ndege mikoani, zingine zinakwenda kwa basi. Hapo nadhani ndiyo hoja ianzie na mjadala ujikite hapo, badala ya kubishana na takwimu na ukweli ulivyo.

Unawezaje kusema ligi na timu ni bora, wakati kama Yanga isingekuwapo kwenye ligi, Simba hii ambayo mastraika wake kufunga ni tatizo ingekuwa bingwa? Nahitimisha mjadala.

# Serikali kueleza kesho mikakati kupoza machungu bei ya mafuta

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

SERIKALI kesho inatarajia kuwasilisha bungeni mikakati ya dharura iliyojiwekea katika kuwanusuru wananchi kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta.

Uamuzi huo ulifikiwa baada ya Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, Alhamisi wiki hii kumwagiza Waziri wa Nishati, January Makamba, kuja na majibu bungeni Mei 10, mwaka huu, kuhusu mkakati wa dharura wa serikali katika kunusuru janga hilo, baada ya mjadala mpana kutoka kwa wabunge waliotaka kufahamu mikakati ya serikali.

Mwishoni mwa wiki mjadala uliibuka bungeni baada ya Mbunge wa Kilindi (CCM), Omary Kigua, kutoa hoja ya kutaka Bunge liahirishwe ili wabunge wajadili suala la kupanda kwa mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa.

Akitoa hoja, Kigua alisema kwa sasa kuna tatizo la kupanda kwa haraka kwa mafuta kulikosababisha kupanda kwa bei ya kila kitu kwa wananchi, kwamba nchi nzima kelele zimekuwa kubwa.

Alisema wabunge wanawajibu wa kusimamia na kuishauri serikali na kwamba wananchi wamewapa dhamana ya kuwasemea na kukaa kimya watakuwa hatuwatendei haki wananchi.

Kigua alisema anafahamu serikali ya CCM ni sikivu na anauhakika ina uwezo wa kufanya kazi na hivyo aliomba wabunge wazungumze kuhusu hoja hiyo ili wasikie serikali inasema nini.

Hoja hiyo ya Kigua iliungwa mkono na wabunge zaidi ya 20, hali iliyomlazimu Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kukubali hoja hiyo kujadiliwa na wabunge.

Hata hivyo, baada ya majadiliano mapana kutoka kwa wabunge ndipo Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alipomuagiza Waziri Makamba kuleta majibu bungeni wiki ijayo kuhusu mkakati wa muda mfupi wa serikali katika kukabiliana na dharura iliyojitokeza nchini.

"Nimewasikia wabunge kuhusu ushauri mlioutoa kwa serikali juu ya kupanda kwa bei ya mafuta. Hivyo serikali itafanya nini katika jambo hili namuagiza Waziri Makamba Jumanne wiki ijayo aje na majibu ya namna ya kutatua jambo hili," alisema Dk. Tulia.

Alisema mkakati wa muda mrefu wa serikali kuhakikisha bei ya mafuta haipandi, itakuja kueleza bungeni siku zijazo.



Ofisa wa Mamlaka ya Bandari akitoa maelezo kwa watu waliotembelea banda la mamlaka hiyo, katika Maonyesho ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi yaliyoandaliwa na OSHA jijini Dodoma hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 5 wafa maji wakivuka kwenda kanisani

**Na Samson Chacha,** RORYA

WATU watano wanaodaiwa ni waumini wa Kanisa la Wasabato wa Kitongoji cha Mori, Kijiji cha Kowak Kata ya Nyathorogo, wilayani Rorya, mkoani Mara wanahofiwa kufa maji baada ya mtumbwi waliokuwa wakivuka kutoka Kitongoji cha Mori kwenda kusali kupinduka.

Waumini hao walikuwa wakienda upande wa pili katika Kijiji cha Matara baada ya kamba iliyokuwa inavuta mtumbwi huo kukatika na kusababisha chombo hicho kupinduka na watu hao wakiwamo wanawake na watoto kufa maji. Wakizungumza na gazeti hili mwishoni mwa wiki Mtendaji wa Kijiji cha Kowak, Charles Mwita na Diwani wa Kata ya Nyathorogo, Godfrey Dalmas, walisema tukio hilo lilitokea Mei 7, mwaka huu, majira ya saa 4 asubuhi katika Mto Mori.

Akisimulia tukio hilo, Mwita alisema mtumbwi huo ulifungwa kamba na ukawa unavutwa na watu waliokuwa ng'ambo ya pili, lakini bahati mbaya ilikatika na chombo hicho kuzama.

Alisema mtumbwi huo ulizidiwa na maji mengi yaliyokuwa yanatiririka ambayo yaliongezeka kutokaa na mvua zinazoendelea kunyesha.

Godfrey alisema miili ya watu wawili akiwamo mtoto wa kike imepatikana na baadhi ya watu waliofika kuokoa waliwataja kuwa ni

Pamela Jaoko na Abuga Rucho, na kwamba jitihada za kutafuta miili mingine zinaendelea.

Viongozi hao walisema katika eneo hilo wamekuwa wakivusha watu kiholela na kwamba mara kwa mara watu hupoteza maisha, na kuiomba serikali kujenga daraja ili kuwasaidia wananchi hao.

Alisema wanaovuka kwenda ng'ambo ya pili kutoka Kitongoji cha Mori kwenda Kijiji cha Matara uvushaji wake unafanyika kiholela na ajali za watu kupelekwa na mto Mori katika eneo hilo ni za mara kwa mara na watu wamepoteza maisha kilio cha wananchi vijiji katika kata ya Nyathorogo ni kujengewa daraja katika kivuko hicho.

# Madai ya wafanyakazi kampuni ya China sasa kushughulikiwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYAKAZI wa kampuni ya Bomet Corporation Limited inayomilikiwa na mwekezaji kutoka China wamelalamikia unyanyasaji ikiwamo kufanya kazi saa za ziada bila malipo na kulazimika kuomba kazi tena baada ya miaka mingi ya kufanya kazi.

Hata hivyo uongozi wa kampuni umesema utayashughulikia masuala ya wafanyakazi hao.

Wafanyakazi hao walisema kuwa licha ya kufanya kazi na kampuni hiyo kwa zaidi ya miaka 14, uongozi wa China uliamua kila mmoja wao kutuma maombi ya kazi tena baada ya Bomet na kampuni dada ya UR Home Company Limited kubadilisha majina kutoka Shikina na Border Limited hivi karibuni.

Wafanyakazi ambao hawakutaka kutajwa majina walisema uongozi wa kampuni ya China pia umewalazimu kusaini hati tupu za malipo ya mishahara kinyume na kanuni.

"Kama watumishi tuna haki ya kupata hati za mishahara ambayo haitumiki hapa badala yake tunasaini vocha tupu," alisema mmoja wa watumishi hao ambaye alihoji sababu za kulipwa mishahara moja kwa moja badala ya kufanya hivyo kupitia akaunti zao za benki.

"Mpangilio huu wote unatufanya tushuku nia ya mwajiri nyuma ya vitendo kama hivyo," mfanyakazi mwingine aliongeza kusema pamoja na wao kupoteza pesa, kuna uwezekano kuwa serikali pia haipati mapato yake.

Kampuni ya Bomet na UR Home ni waagizaji wa bidhaa mbalimbali zikiwamo nguo, nepi, samani, vifaa vya ujenzi na bidhaa za baharini zenye makao makuu yake jijini Dar es Salaam na ghala lililopo Chang'ombe Temeke.

Akijibu tuhuma zilizotolewa na wafanyakazi hao, mmoja wa Mameneja wa mtaa wa Bomet, Samuel Mbogo alisema uongozi utaangalia tuhuma hizo na kuchukua hatua stahiki. "Tumesikia malalamiko ya wafanyakazi na tunachunguza ili kubaini ukweli kabla hatua hazijachukuliwa," alisema Mbogo.

Alidokeza kuwa wakati huo huo, usimamizi wa Bomet na UR Home unafanya kazi kwa bidii ili kuboresha mazingira ya kazi ambayo yameathiriwa na kupanda kwa bei ya vifaa vya kimataifa na vikwazo vya ugavi.

"Baadhi ya malalamiko hayo yanatokana na changamoto za soko ambazo tunakabiliana nazo kama kampuni na itachukua muda kushughulikia," alidokeza huku akiwataka wafanyakazi kuwa watulivu wakati usimamizi unashughulikia shida zao.



Paroko wa Parokia ya Mtakatifu Tom Mtume - Muungano, George Sai (wapili kulia), akipanda mti ili kutunza mazingira hafla iliyoambatana na uzinduzi wa Jubilei ya miaka 50 ya Jumuiya ya Wanawake Wakatoliki (WAWATA) iliyofanyika kanisani hapo, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Msaidizi wa Paroko, Gabriel Kpohihin. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bunge laagiza kutengwa maeneo ya wamachinga

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

BUNGE limeiagiza serikali kuhakikisha linatenga maeneo maalumu ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara wadogo 'machinga'.

Limeagiza kuwa maeneo hayo yanapaswa kuwa wezeshi na rafiki kwa wananchi kufika ili wafanyabiashara hao waweze kupata soko la kuuza bidhaa zao.

Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Martha Gwau, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki bungeni wakati akisoma taarifa ya kamati hiyo, kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara pamoja na maoni.

Serikali kupitia wakuu wa mikoa mbalimbali ilitangaza mpango mkakati wa kuondoa adha ya wafanyabiashara wadogo walioweka vibanda juu ya mifereji ya maji, katika njia za wapita kwa miguu, hifadhi za barabara na mbele ya maeneo ya taasisi za umma kama shuleni.

Akiwasilisha maoni ya kamati hiyo, Gwau alisema: "Kuhusu utengaji wa maeneo ya kufanya biashara kwa wafanyabiashara madogo (machinga); serikali imefanikiwa kuchukua hatua za makusudi katika kuweka mazingira wezeshi dhidi ya kundi hilo.

"Kamati inatoa rai kwa serikali kuhakikisha machinga nchi nzima wanapatiwa maeneo ya kufanyia biashara.

Aidha, maeneo hayo yawe wezeshi na rafiki kwa watu kufika ili wamachinga hawa waweze kupata soko la kuuza bidhaa zao." Gwau ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum alisema vilevile viongozi wa mikoa na halmashauri wanapaswa kuwaongoza machinga vizuri katika kuwapanga, kuhakikisha mazingira yao yanakuwa salama muda wote.

Kuhusu uboreshaji wa mazingira ya biashara nchini na uwekezaji, Gwau alisema: "Pamoja na mafanikio na jitihada za serikali kufuta na kupunguza jumla ya ada na tozo 60 ambazo zilikuwa zinatozwa na wizara, idara na taasisi zinazojitegemea.

"Kamati inazidi kuweka msisitizo kwa serikali kuendelea kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na mfumo funganishi ili kuondoa kabisa adha kwa wawekezaji kupata huduma kwa haraka."

Kuhusu uandaaji wa kanzidata ya viwanda, Gwau alisema kamati inasisitiza kanzidata hiyo iwe na hifadhi ya mkusanyiko wa taarifa na takwimu zilizochakatwa na kupangwa kwa namna inayorahisisha upatikanaji wa taarifa hizo, kuzitunza, kuzisimamia na kuzisafisha.

Alisema kanzidata hiyo ni muhimu kwa kuwa itasaidia katika kufahamu na kupata taarifa sahihi, za uhakika na kwa wakati kuhusu idadi ya viwanda, ujuzi, ajira na bidhaa zinazozalishwa nchini.

# Uwekezaji kwenye nishati wafunguliwa milango

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewaalika wawekezaji wa ndani na nje ya nchi kuwekeza katika fursa lukuki zilizoko kwenye sekta ya nishati ambayo ni muhimu katika uendeshaji wa mitambo na mashine mbalimbali viwandani.

Wito huo wa serikali ulitolewa kwenye mkutano wa kuhitimisha ziara ya kundi la wafanyabiashara kutoka mataifa ya Norway na Uingereza ambao walikuwapo nchini tangu Mei 3, mwaka huu, kwa lengo la kujadiliana namna ya kubaini fursa mpya za uwekezaji zinazopatikana nchini.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji, anayeshughulikia Uwekezaji, Ally Gugu, alisema Tanzania ina fursa nyingi katika eneo la nishati na zinahitaji uwekezaji.

Gugu alisema serikali imeendelea kufungua milango ya wawekezaji katika sekta mbalimbali husasani nishati ambayo ndio kiini kikubwa katika kukuza uchumi wa nchi hasa katika kipindi hiki ambacho serikali imejielekeza katika uchumi wa viwanda.

Alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya nishati asilia vikiwamo jua, gesi, maji, upepo, ambavyo ni rafiki katika utunzaji wa mazingira na endapo wawekezaji wakitumia fursa hiyo wanaweza kuzalisha umeme mkubwa ambao utakuwa na tija katika maendeleo ya viwanda nchini.

"Nchi yetu imebarikiwa kuwa na fursa nyingi za uwekezaji kwenye masuala yanayohusu nishati, tuna maji ya kutosha, tuna jua, upepo, gesi, taka, tunawaalika wawekezaji wote wa ndani na nje kuzitumia fulsa zilizopo hasa kipindi hiki ambacho serikali imewekeza nguvu katika maendeleo ya viwanda," alisema Gugu.

Alimshukuru Rais Samia Suluh Hassan ambaye amekuwa kipaumbele katika kuhamasisha wawekezaji na kutangaza fursa zilizoko nchini katika mataifa mbalimbali duniani hasa kupitia filamu ya ROYAL TOUR, ambapo kupitia ushawishi wake nchi imepokea wageni wengi wenye nia ya kuwekeza na tayari miradi 37 kutoka Dubai imesha-sainiwa.

Naye Balozi wa Norway nchini, Elisabeth Jacobsen, alieleza kuridhishwa na mahusiano mazuri ya kibiashara yaliyopo kati ya nchi hizo mbili ambayo yalianza mwaka 1970 na yamedumu kwa takribani miaka 50, amabyo uwekezaji wake ulijikita katika kufanya upembuzi na kutafiti rasilimali za umeme Tanzania.

"Tanzania na Norway ni nchi zenye mahusiano imara na ya kihistoria katika uwekezaji wa nishati, mahusiano yetu yalianza miaka 50 iliyopita tumefanya kazi pamoja na tumefanikiwa pamoja kuimarishsa uwezo wa watumishi, kubuni na kujenga mitambo mikubwa ya umeme na kusambaza katika maeneo mbalimbali hasa ya vijijini," alisema Elisabeth.

# Wabunge wataja mbinu kunusuru mfumuko bei

**Na Gwamaka Alipipi,**
DODOMA

KUTOKANA na kuwapo kwa mfumuko wa bei ya bidhaa hususani mafuta ya kula, wabunge wameishauri serikali kujielekeza katika uwekezaji wa mashamba makubwa ya alizeti pamoja na kupunguza kodi katika bidhaa.

Wamesema serikali inapaswa kufanya uwekezaji wa miaka 10 kwenye kilimo cha alizeti hali itakayosaidia nchi kuondokana na uagizaji wa mafuta kutoka nje na kupanda kwa bei.

Waliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wakichangia makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2022/23 ambayo imetengewa Sh.bilioni 99.105.

Mbunge wa Singida Magharibi (CCM), Elibariki Kingu, alisema: "Hivi hadi karne hii Tanzania bado tunaagiza mafuta ya kula kutoka nje? Hili Taifa halikutakiwa kuagiza mafuta kabisa kutokana na ardhi tuliyonayo. Wizara ya Viwanda na Biashara fanyeni co-ordination (ushirikiano) ndani ya miaka 10 tutaondokana na uagizaji wa mafuta ya kula."

Aliongeza: "Hivi Tanzania tunashindwa kuwa na uzalishaji wa mafuta? Sisi leo ni wa kulia? Ardhi nzuri Mungu ametupa. Tatizo tuna plan sana, lakini hatuchukui hatua. Kwa mfano tukiwa na mashamba ya alizeti makubwa hatutaweza kuagiza mafuta ya kula."

Alisema Taifa lazima liwe na vipaumbele vichache vitakavyoipa sifa Tanzania.

Mbunge wa Viti Maalum, Salome Makamba alisema nchi nyingi zilizoendelea zimewekeza kwenye Wizara ya Viwanda na Biashara kwa sababu yenyewe ndiyo kichocheo cha uchumi.

Mbunge wa Viti Maalum CCM, Subira Mgalu, alisema: "Kumekuwa na kupanda kwa bie ya bidhaa kwa Watanzania. Serikali iliangalie jambo hili kwa mapana."

Mbunge wa Ndanda (CCM), Cecil Mwambe alisema kwa sasa kuna mfumuko wa bei mkubwa hususani mafuta ya kula, kwamba wafanyabiashara wanapandisha bei ya bidhaa kiholela.

Mbunge wa Nkasi Kaskazini (CHADEMA), Aida Khenani, alisema kwa sasa mitaji ya wafanyabiashara imeshuka kwa sababu ya utitiri wa kodi, kwamba hali hiyo ikiendelea maduka yatafungwa.

Alisema ni wakati mwafaka kwa serikali kuchukua hatia kunusuru hali hiyo, kwamba kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu kupanda kwa bidhaa.

Hata hivyo, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, wakati akiwasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka 2022/23 alisema kutokana na athari za UVIKO-19, vita kati ya Urusi na Ukraine, ugavi wa mazao na bidhaa unaendelea kuathiri bei za bidhaa mbalimbali za viwandani hususani zile zinazotegemea malighafi kutoka nje au kuagizwa kutoka nje zikiwamo mafuta ya kula, mafuta ya petroli na ngano.

Alisema hali hiyo inatokana na utegemezi wa biashara ya malighafi na bidhaa hizo ambazo uzalishaji na usambazaji wake unaguswa na uchumi wa nchi hizo, kwamba hali hiyo itaathiri urari wa biashara kutokana na kuyumba kwa biashara katika masoko hayo ikiwianishwa na uwezo wa kulipia bidhaa kutoka nje.

Alisema katika kukabiliana na changamoto hizo, serikali imechukua hatua zenye matokeo ya muda mfupi na muda mrefu.

Dk. Kijaji alisema kwa kuhusu mafuta ya kula ya alizeti, katika Mkataba wa Makubaliano (MoU) ya uwekezaji yaliyofikiwa mwaka huu Marekani, kuna mkataba wa mradi wa kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula (Kitaraka - Manyoni), ambao utachochea jitihada za serikali kuhakikisha kuwa inaimarisha uzalishaji wa bidhaa hizo ambazo tunategemea soko la nje.

Waziri Kijaji alisema: "Aidha, Waziri Mkuu aliagiza TARI kugawa miche ya kisasa ya michikichi huko Kigoma, ili kuongeza uzalishaji. Vilevile, mikoa ya Singida, Dodoma na Simiyu ni mikoa ya kimkakati ya kuzalisha alizeti ili kuongeza upatikanaji wa mafuta ya kula nchini.

"Pia wizara kupitia SIDO itajenga viwanda viwili vidogo vya kuzalisha mafuta ya mawese katika Kijiji cha Nyamuhoza kilichoko kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Kigoma na Kijiji cha Sunura kilichoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Ujiji.

# Mamia ya kaya Ilala zaunganishwa mfumo uondoshaji majitaka

**Na Joseph Mwendapole**

KAYA 171 za Mtaa wa Kisiwani, Kata ya Buguruni, Wilaya ya Ilala, jijini Dar es Salaam zimeunganishwa katika mfumo rahisi wa uondoshaji majitaka kwenye makazi ya watu kwa lengo la kuimarisha usafi wa mazingira.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Msimamizi wa Miradi wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Mhandisi Fredrick Mujungu.

Alikuwa akizungumza wakati wa mkutano ulioandaliwa na mamlaka hiyo kwa ajili ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa mradi huo ambapo alisema mradi huo ni jitihada za serikali kupitia DAWASA za kuboresha usafi wa mazingira kwenye makazi ya watu wengi wenye kipato cha chini.

"Mradi huu unatoa picha halisi ya sifa za choo bora ikiwamo kuta imara na zenye rangi, mlango imara, paa lenye kusitiri na linaloruhusu hewa kuingia, sakafu bora isiyoruhusu maji kutuhama pamoja na usafi unaoridhisha," alisema.

Mhandisi Mujungu alisema hiyo ni awamu ya kwanza ya mradi na kazi inayoendelea sasa ni kuhamasisha wakazi wengine wajiunge kwenye mfumo huo na kwamba kata 82 bado hazijajiunga kwenye huduma hiyo.

"Nitoe rai kwa ambao bado hawajiunga kufanya hivyo kwa kuwa mradi huu una manufaa mengi na gharama yake ni nafuu ya shilingi 5,600 tu kwa mwezi kwa kaya moja," alisema.

Kwa upande wake Ofisa Afya wa Kata ya Buguruni, Renatus Rwehabura, alisema kila mwananchi anawajibika kisheria kuhakikisha anakuwa na choo bora na salama kwa afya yake na mazingira yanayomzunguka.

"Lazima ifahamike kuwa mtu yeyote anayekiuka anaweza kuchukuliwa hatua ikiwamo kulipa faini ya shilingi 200,000," alisisitiza.

Naye Mwenyekiti wa Mtaa huo, Uwesu Uwesu, aliwataka wananchi ambao bado hawajajiunga kwenye mfumo kufanya hivyo na kabla ya Juni 30 mwaka huu na kwamba watakaoshindwa kufanya hivyo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Mradi huu una manufaa makubwa kwa wananchi na serikali imetujali sana mpaka kutujengea vyoo sisi wananchi wake, hivyo ni vyema na sisi tukathamini jambo hili jema kwa kujiunga kwenye mfumo na kuwa na matumizi bora ya choo ili kuimarisha usafi wa mazingira kwani ndio usalama wetu," alisema.

Mkazi wa Mtaa huo ambaye ni mnufaika, Ramadhan Kiwinga, alisema awali choo chake cha shimo kilikuwa kinajaa mara kwa mara na kuchafua mazingira hivyo kulazimika kuingia gharama kubwa ya kunyonya majitaka.

"Lakini tangu nilipojiunga kwenye mfumo rahisi wa mradi huu wa DAWASA, nimepata unafuu mkubwa, kwa sasa hamna uchafu, choo kisafi na gharama za uondoshwaji ni nafuu sana tofauti na awali," alisema.




Ofisa Habari wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini (TCAA), Ally Changwila, akitoa elimu kwa wakazi wa Mkoa wa Arusha waliofika kwenye mamlaka hiyo kwenye maonyesho ya Wiki ya Ununuzi wa Umma katika viwanja vya AICC. **PICHA: TCAA**

# Watakiwa kutowaficha watoto wenye ulemavu siku ya sensa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MBUNGE wa Jimbo la Ushetu (CCM), Emmanuel Cherehani, amewataka wananchi kutowaficha watoto wao hususani wenye ulemavu wakati wa siku ya sensa ya watu na makazi kwa kuwa kufanya hivyo ni kwenda kinyume na haki za binadamu.

Cherehani alitoa kauli hiyo katika mikutano ya hadhara uliofanyika kata za Uyogo na Bukomela, Halmashauri ya Ushetu, wakati akisikiliza na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili wananchi wa jimbo lake, alisema sensa hufanyika kila baada ya miaka 10.

Alisema, hapo awali Wilaya ya Kahama ilikuwa na jimbo moja la Kahama na baada ya kufanya sensa ya watu na makazi mwaka 2012 yalipatikana majimbo mengine matatu likiwamo Ushetu na Msalala.

Cherehani alisema, sensa inatarajia kufanyika Agosti 23, mwaka huu nchi nzima na jukumu lilipo kwa sasa ni wenyeviti wa vijiji, mitaa kwa kushirikiana maofisa wa maendeleo jamii kuendelea kutoa elimu ya muhimu wa sensa kwa wananchi.

Aidha, aliwataka wananchi wa Jimbo la Ushetu kuwapuuza wanaopita na kuwahamasisha kutoshiriki sensa na badala yake wawaripoti kwa viongozi wao ili wachukuliwe hatua za kisheria, itakapotangazwa vijana wenye sifa wajitokeze kuomba kwa kuwa ni sehemu ya ajira za muda.

Naye Mtendaji wa Kijiji cha Kabila, James Mumba alisema, kwa sasa wanasubiria miongozo ya utekelezaji wa sensa ya watu na makazi kutoka halmashauri na sasa wanaendelea kutoa elimu ya umuhimu wake kupitia vikao mbalimbali.

Katika vikao vya maendeleo ya kata moja ya ajenda wanayojadili ni kuhamasisha kila mmoja kwa nafasi yake kusisitiza wananchi kujitokeza kuhesabiwa siku ya sensa na watoto wote husuani wenye ulemavu kuhesabiwa.

Mkazi wa Uyogo, Rose Malilo alisema, ameshiriki sensa mbalimbali tangu mwaka 1988 mpaka mwaka 2012 na kwamba viongozi wa serikali wasisite kumshirikisha kuwahamasisha wananchi kujitokeza kuhesabiwa kwa kuwa umuhimu wake anaufahamu.

# SBL yapata tuzo kusaidia elimu ya ufundi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Bia ya Serengeti (SBL) imepata tuzo ya heshima na kutambuliwa kutokana na mchango wake katika kusaidia maendeleo ya elimu ya ufundi nchini.

Kampuni hiyo ilipata tuzo hiyo hivi karibuni jijini Dar es Salaam kupitia programu yake ya Kilimo Viwanda ambayo hutoa ufadhili ya masomo ya kilimo kwa wanafunzi wenye uwezo mzuri darasani na ambao wanatoka familia zenye kipato duni.

Tuzo hiyo ilitokana na utafiti uliofanywa na Baraza la Elimu ya Ufundi Tanzania (NACTVET) kwa kushirikiana na Taasisi ya Waajiri (ATE) pamoja na Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF) uliolenga kuwatambua waajiri wanaosaidia maendeleo ya elimu ya ufundi.

Akizungumza baada ya kupokea tuzo hiyo, Meneja Uhusiano kwa Serikali wa SBL, Neema Temba, aliwashukuru waandaaji wa tuzo hizo na kusema kuwa ni jambo la faraja kuona kuwa SBL jitihada za SBL katika kusaidia jamii zinatambulika.

"Ni furaha kubwa kwetu sisi SBL kupata tuzo hii. Tuzo hii ni ushahidi mzuri kuwa programu zetu zinaigusa jamii ya Watanzania na ndiyo maana leo hii tumweza kutambuliwa kwa kupewa tuzo," alisema.

Neema alisema kilimo viwanda ni programu iliyobuniwa na SBL kwa ajili ya kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kilimo ambao wana uwezo mkubwa darasania na ambao wanatoka katika familia masikini.

"Tangu kuanza kwa programu hii mwaka 2020, tayari zaidi ya wanafunzi 200 wamenufuika. Kupitia programu hii, wananufaika hulipiwa ana na gharama zote za masoko kwa kipindi chote wanachokuwa masomoni," alifafanua.

Alisema SBL kupitia kilimo viwanda imekuwa ikiunga mkono jitihada za serikali za kuongeza wataalamu wa kilimo ambao ni nguvu muhimu katika kuongeza tija kwenye kilimo ambacho ndiyo sekta mama kwa Tanzania.

# Gwajima awafunda wazazi kuhusu malezi

Na Sabato Kasika

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. Dorothy Gwajima, amewataka wazazi na walezi kuhakikisha wanakuwa na mazungumzo yenye weledi kwenye familia zao, kwa kuwa yanasaidia kuleta maelewamo na mashikamano wa familia.

Alisema, mazungumzo hayo pia yanasaidia kuleta maendeleo ya kiuchumi kwa familia na maendeleo ya mtoto katika nyanja za elimu, lishe, afya, maadili na utamaduni na yanaimarisha ulinzi kwa mtoto dhidi ya vitendo vya ukatili vinavyoendelea kuongezeka nchini.

Waziri Gwajima alisma hayo Mbezi Luis Manispaa ya Ubungo Dar es Salaam juzi, alipokuwa akizungumza na wananchi wa eneo hilo, katika ziara yake ya maadhimisho ya Siku ya Familia Duniani inayofikia kilele chaka Mei 15 mwaka huu.

"Siku ya Familia Duniani itakuwa na maana zaidi kama wazazi, walezi na jamii itazungumza kwa waledi, kwa lengo la kuimarisha umoja na mshikamano kwenye familia," alisema Dk. Gwajima.

Alisema, inakadiriwa kuwa, ukatili kwa watoto umekuwa ukiripotiwa kufanyika zaidi nyumbani kwa asilimia 60 na shuleni kwa asilimia 40 kutokana na kutokuwapo kwa mazungumzo yenye weledi.

"Hayo ni kwa mujibu wa Taarifa ya Hali ya Ukatili dhidi ya Watoto ya mwaka 2011 iliyofanywa na serikali kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa (UNICEF)," alisema.

Alifafanua kuwa Siku ya Familia Duniani, mwaka huu kila mkoa utaadhimishwa kwenye eneo lake kwa kuzingatia maelekezo ya wizara yake ikiwamo kuitisha makongamano ya kujadili namna ya kuisaidia jamii katika malezi ya familia ili kuwa na familia bora na zenye ustawi.

"Kwa upande wetu sisi kama wizara, tutaungana na Mkoa wa Dodoma, yalipo makao makuu ya nchi, ambapo mgeni rasmi atakuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa," alisema.

Dk. Gajima alisema, kwa kuwa maadhimisho ya mwaka yataangukia siku ya Jumapili ambayo ni ya mapumziko, aliwataka wazazi kutumia siku hiyo kukaa karibu na familia zao na kutafakari na kuzungumza pamoja juu ya maendeleo na ustawi wa familia zao huku wakifuatilia vipindi mbalimbali vya maadhimisho.

Ili kuimarisha maadili katika familia, mkazi wa Mbezi aliyejitambulisha kwa jina la Robart Lucas, alishauri jamii kuacha kuiga utamaduni wa nchi za magharibi ambao alidai umeachangia kuharibu vijana.

"Unakuta katika TV kuna vipindi ambavyo havifai, lakini vijana wadogo na hata watoto wanaviangalia, mwisho wake kumomonyoka kwa maadili na hata kusababisha mambo ya ukatili wa kijinsia," alisema Lucas.

Mwajuma Debwe kwa upande wake alimwambia waziri kuwa wazazi na walezi wamekuwa na majukumu mengine yanayosababisha kulegalega kwa malezi ya familia hadi watoto kuharibika.

"Lakini pia ipo haja kwa jamii kubadili mtindo wa maisha ikiwamo kutambua kuwa malezi ya mtoto si familia tu bali ni la jamii nzima, na ndivyo ilivyokuwa enzi zetu wa makuzi yetu," alisema Mwajuma.

Alifafanua kuwa enzi hizo haikuwa rahisi mtoto kumpita mtu mzima bila kumsalimia au kumpokea mzigo, kumpisha kiti katika vyombo vya usafiri, na kwamba malezi kwa sasa yapotea ndani ya jamii.

Mzazi huyo aliongeza kuwa si hayo tu bali pia suala la kamari limeteka watoto wengi kutokana na wazazi kutokuwa na muda wa kukaa na waatoto wao ili kujua maendeleo yao.

"Watoto wanakwenda kwenye majumba ya sinema, wazazi wakiambia kuhusu hali hiyo, lakini pia niwaombe wazazi wenzangu na serikali yetu, siku hii ya maadhimisho ya Siku ya Familia yasiwe yansubiri Mei 15 tu bali tufanye kila Jumamosi iwe siku ya familia," alisema.

Siku ya Familia Duniani kwa mwaka huu wa 2022, inaongozwa na kaulimbiu isemayo; 'Dumisha Amani na Upendo kwa Familia Imara;




Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale mkoani Geita, Jamhuri David (kulia), akishiriki kuzoa taka baada ya kupokea trekta ya kusomba takataka yenye thamani ya Sh. milioni 78 iliyotolewa na mgodi wa Barrick Bulyanhulu kwa halmashauri ya wilaya hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tigo yadhamiria kufika vijijini

Na Jenifer Gilla

KATIKA kuhakikisha kuwa inafikisha huduma za mawasiliano vijijini kampuni ya Tigo imetenga zaidi ya Sh. trilioni moja kupeleka mawasiliano vijijini.

Hayo yalibainishwa na wamiliki wapya wa kampuni hiyo, mfanyabiashara Rostam Aziz Hassanein Hiridjee, walioongea na waandishi wa habari kuhusu madhumuni ya ushirikiano wao katika biashara hiyo.

Rostam alisema mpango huo una lengo la kuiunga serikali mkono katika adhma ya kuhakikisha wanaifikia asilimia 60 ya Watanzania ambao wapo vijijini.

"Tumetenga zaidi ya Sh. trilioni moja kuhakikisha Tigo inafika vijijini kuinua biashara za watu na kuwapa huduma bora," alisema Rostam.

Uwekezaji wa fedha hizo, alisema utafanywa ndani ya miezi 18 ijayo kutegemea ushauri utakaotolewa na wataalamu wa mawasiliano waliopo ndani ya kampuni hiyo waliyoinunua mwezi uliopita.

Vilevile Rostam alisema kuna faida kubwa ya uwekezaji ukishirikisha wazawa kwa sababu pesa nyingi itabaki nyumbani tofauti na akiwemo mwekezaji kutoka nje peke yake.

Aliwataka Watanzania kufurahia mafanikio ya kila Mtanzania anayeshiriki biashara kubwa na kuondokana na kasumba ya kuiacha miradi hiyo kwa wageni kutoka nje.

Rostam alisema kwa muda mrefu Watanzania walizoea kuwakaribisha wageni kunufaika na rasilimali zilizopo, lakini kipindi hicho kimekwisha na sasa utaratibu unatakiwa kubadilika kwa kujipanga kushirikiana nao.

"Kuwa na wawekezaji kutoka nje hakukwepeki kwa sababu wao wana mitaji mikubwa, ila wakiwamo wazawa manufaa yake huwa makubwa zaidi. Mtanzania mmoja akifanikiwa, tushangilie. Hata watendaji wa serikali, nawaomba wakimwona mtu anahangaika kufanikisha biashara yake, wamsaidie," alisema.

"Mimi nitazitumia na ndugu zangu wa Igunga pamoja na marafiki zangu waliopo maeneo tofauti nchini. Mimi ni muumini wa ajira kwa Watanzania pia, wao pia watanufaika," alisema Rostam.

Naye mwenyekiti wa Axian Group, yenye makao makuu visiwa vya Madagascar, Hiridjee alisema alivutiwa kufanya uwekezaji huo nchini baada ya kufanya mazungumzo na mwenyeji wake Rosta, kwa saa sita mfululizo.

"Alinipa sharti moja kwamba uwekezaji huu lazima ulinufaishe Taifa kwanza kabla ya Rostam mwenyewe. Nilikubaliana naye kwa sababu ndio kitu tunachokifanya katika mataifa yote tulikowekeza. Huu ni uwekezaji wa Watanzania utakaoendeshwa na Watanzania, ili kuwanufaisha Watanzania," alisema Hiridjee.

Alieleza kilichomvutia nchini kuwa ni kasi na uimara wa uchumi, uelewa na elimu ya wananchi pamoja na hamasa ya kuwakaribisha wageni inayofanywa na serikali.

# Benki yawapunguzia riba ya mikopo watumishi wa umma

Na Mwandishi Wetu

WATUMISHI wa umma wamepata fursa baada ya kupunguziwa riba ya mikopo.

Fursa hiyo kwao imetolewa na Benki ya Stanbic Tanzania ambayo imesema inaendelea kusaidia wateja wao kutimiza ndoto zao kwa kutoa suluhisho za kifedha zinazokidhi mahitaji yao.

Benki hiyo imetangaza kuwa imepunguza kiwango cha riba kwenye mikopo ya mishahara isiyo na dhamana kwa watumishi wa umma hadi asilimia 12.5 katika kampeni itakayoendeshwa kwa miezi mitatu.

Kiwango hiki kipya cha riba kutoka benki hiyo kinakuja wakati serikali imekuwa ikifanya juhudi za kimkakati kudumisha ukuaji wa uchumi licha ya athari za janga la UVIKO-19 na ulimwengu kukabiliwa na kupanda kwa bei ya mafuta na bidhaa tofauti.

Akitoa ufafanuzi wa kampeni hiyo Mkuu wa Wateja Binafsi, Omari Mtiga alisema: "Kwa muda wa miezi mitatu wafanyakazi wa sekta ya umma wanaweza kupata mikopo ya mshahara isiyokuwa na dhamana kwa riba ya asilimia 12.5 ambayo itatolewa ndani ya saa 48 za kazi.

Lengo letu ni kuhakikisha kuwa mikopo yetu inatoka kwa haraka na bila vikwazo ili kuhakikisha kuwa wateja wetu wanaweza kufaidika kikamilifu kipindi cha kampeni."

Aliongeza kuwa benki hiyo imeamua kupunguza riba ili kutoa mikopo kwa wateja wake wa sekta ya umma jambo ambalo litasaidia kukuza kipato chao na uchumi wa taifa kwa ujumla.

"Tumedhamiria kuwasaidia watumishi wa umma kwa kuwapunguzia mzigo wa kifedha kwa kuwapatia mikopo yenye masharti nafuu ili kuwawezesha kutimiza ndoto zao kwa sababu tunatambua na kuthamini juhudi kubwa wanazoziweka katika kuitumikia jamii," alisema.

NIPASHE JUMATATU MEI 9, 2022

Nipashe

Spotika



WACHEZAJI 10 BORA WA SOKA WA WAKATI WOTE UK. 12-13




# MAKOCHA 6 AMBAO HAWAJAWAHI KUFUKUZWA

## ISIKUPITE

ALAN Shearer, bado anabaki kuwa mchezaji pekee katika Ligi Kuu England anayeshikilia rekodi ya kufunga mabao mengi (260), akifanya hivyo kati ya mwaka 1992 na 2006, ambayo yametokana na jumla ya mechi 441 alizocheza akiwa na Blackburn Rovers (1992-1996) na Newcastle United (1996-2006).



**LONDON,** England

KUSIMAMIA klabu ya mpira wa miguu si kazi rahisi. Mpira wa miguu ni mchezo unaozingatia matokeo kwa kiwango kikubwa kutokana na kiasi kikubwa cha fedha kinachowekezwa. Kuanzia kuweka ari kwenye vyumba vya kubadilishia nguo hadi kuhakikisha wachezaji wanaofaa wamesajiliwa, huku kocha akiwa na kazi yake.

Kuwa kocha wa mpira wa miguu kwa hakika ni hatari kubwa, kazi yenye malipo ya juu, hasa katika ngazi ya juu. Makocha wanaabudiwa na hutafutwa wanapotoa matokeo mazuri na kushinda mataji. Lakini, mara nyingi hufukuzwa kwa kushindwa kutoa matokeo chanya, kushuka kwa kiwango, au hata kugombana na wachezaji au uongozi.

Ingawa kufukuza makocha kumekuwa sehemu ya mpira wa miguu kwa muda mrefu, kiwango hicho kimeongezeka kwa kiasi kikubwa katika miongo miwili iliyopita. Timu huwa zinatafuta mafanikio, yawe ya muda mfupi au mrefu. Chelsea ni mfano bora, huku 'The Blues' hao wakiwatimua makocha 15 tangu mwanzo wa karne hii. Pamoja na hayo kusemwa, baadhi ya makocha hawajawahi kufutwa kazi, na hawa ni sita kati yao...

### #6. Julian Nagelsmann

Julian Nagelsmann ni mmoja wa makocha bora wachanga duniani. Akiwa ameonja mafanikio katika klabu ya 1899 Hoffenheim na RB Leipzig. Nagelsmann alichukua mikoba ya Bayern Munich mwanzoni mwa msimu. Kwa kweli ni ngumu kuamini katika umri wake wa miaka 34 anasimamia moja ya klabu kubwa duniani.

Mjerumani huyo kipindi chake cha uchezaji alikabiliwa na majeraha, ambapo aliacha kucheza akiwa na umri mdogo wa miaka 20. Kisha aliamua kuelekeza umakini wake kwenye ukocha. Wakati wa siku zake za mapema katika ukocha, Nagelsmann alimsaidia Thomas Tuchel katika klabu ya FC Augsburg.

Nagelsmann, ambaye aliitwa "kocha Bora wa mpira wa miguu wa Ujerumani" mwaka 2017, hajawahi kutimuliwa katika maisha yake ya ukocha.

### #5. Didier Deschamps

Didier Deschamps anasifika kwa kuiongoza Ufaransa kutwaa taji la Kombe la Dunia la FIFA la 2018. Kocha huyo mwenye umri wa miaka 53, alikuwa mchezaji wa soka wa kutisha enzi zake za uchezaji. Alishinda kila kitu akiwa na Ufaransa na alikuwa mshindi mfululizo kule Marseille na Juventus pia. Deschamps hata aliiongoza Monaco kutinga fainali ya kwanza na ya pekee ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2014, na hatimaye kushindwa na FC Porto iliyokuwa ikinolewa na Jose Mourinho.

Aliteuliwa kuwa kocha wa Ufaransa baada ya Euro 2012 na amekuwa hapo kwa takriban muongo mmoja sasa. Ufaransa wameshinda Kombe la Dunia, Ligi ya Mataifa ya Uefa, na kumaliza washindi wa pili kwenye Euro 2016.

Kabla ya kuinoa timu ya taifa, Deschamps alifundisha Monaco, Juventus, na Marseille. Gwiji huyo hajawahi kufukuzwa kazi. Yeye pia ni mmoja wa wanaume watatu pekee walioshinda Kombe la Dunia kama mchezaji na kocha pamoja na Mario Zagallo na Franz Beckenbauer.

### #4. Luis Enrique

Luis Enrique, kama Didier Deschamps, pia ameweza katika ngazi ya klabu na nchi. Enrique alianza maisha yake ya ukocha akiwa na Barcelona B kabla ya kuzifundisha AS Roma, Celta Vigo na Barcelona. Alifurahia miaka mitatu yenye matunda na wababe hao wa Katalunya kati ya 2014 na 2017.

Kocha huyo wa Hispania aliisaidia Barca kushinda mataji mawili ya LaLiga, mataji matatu ya Copa del Rey (Kombe la Mfalme) na taji moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Kocha huyo mwenye umri wa miaka 51, amefanya kazi nzuri kwa timu ya taifa ya Hispania pia. Hispania ilikosolewa vikali kwa uteuzi wao wenye utata kabla ya Euro 2020. Hata hivyo, bado walifanikiwa kutinga nusu fainali.

### #3. Zinedine Zidane

Zinedine Zidane anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora katika historia ya mpira wa miguu. Ingawa wachezaji wengi wa hadhi ya juu duniani hawajapata ushindi katika nafasi zao za uongozi. Zidane amefanya maajabu. Mfaransa huyo ameshinda mataji mawili ya LaLiga na mataji matatu mfululizo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid.

Zidane alishinda yote kama mchezaji katika ngazi ya klabu na nchi. Ni vigumu kulinganisha mafanikio yake na makocha kama Pep Guardiola na Jurgen Klopp kwa sababu za wazi. Ingawa wawili hao ni bora zaidi kimbinu, Zidane anajulikana kwa ustadi wake wa kusimamia watu.

Mshindi huyo wa Ballon d'Or amekuwa na misimu miwili tofauti Santiago Bernabeu akiwa kocha. Hata hivyo, hakufukuzwa katika vipindi vyote viwili, huku Mfaransa huyo akijiuzulu mara zote mbili.

### #2. Pep Guardiola

Pep Guardiola ni mmoja wa makocha bora wa karne ya 21. Raia huyo wa Hispania mwenye uwezo mkubwa ameziongoza Barcelona, Bayern Munich na Manchester City, akitawala ligi ya nyumbani katika vipindi vyote vitatu.

Licha ya kusimamia klabu tatu tofauti zaidi katika soka duniani, Guardiola hajawahi kutimuliwa. Kocha huyo mwenye umri wa miaka 51, alikuwa na nia ya kujipa changamoto katika mazingira tofauti, hivyo akaiacha Barcelona na kuelekea Bayern Munich, ambayo aliiacha na kwenda kuinoa Man City.

Hata hivyo, imekuwa zaidi ya muongo mmoja tangu anyanyue taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. Lawama nyingine dhidi yake ni kwamba huwa anasimamia klabu kubwa badala ya kwenda kwenye timu ndogo na kuziboresha. Pamoja na hayo yote kusemwa, Guardiola bado ni mmoja wa makocha bora wa wakati wote.

### #1. Jurgen Klopp

Jurgen Klopp, pamoja na Pep Guardiola aliyetajwa hapo juu, amekuwa mmoja wa makocha bora kwenye mpira wa miguu dunia katika siku za hivi karibuni. Liverpool na Manchester City wametawala soka la Uingereza.

Tofauti na majina mengi kwenye orodha hii, kocha huyu wa Ujerumani alikuwa na kipindi kifupi cha uchezaji, lakini aliishia kuwa kocha mzuri. Klopp alianza kazi yake ya ukocha huko Mainz kabla ya kuinoa Borussia Dortmund.

Ameipeleka Liverpool fainali moja ya Ligi ya Europa na fainali mbili za Ligi ya Mabingwa Ulaya ndani ya miaka mitano, akishinda moja na Ligi Kuu. Pia ameshinda Kombe la Super Cup na Kombe la Klabu Bingwa ya dunia.

Tofauti na mpinzani wake Guardiola, Klopp hajawahi kuwa na bajeti nyingi zaidi ya kufanya kazi naye. Zaidi ya hayo, kocha huyo wa Liverpool hatimaye alimaliza kusubiri kwa muda mrefu kwa 'Wekundu' hao kutwaa taji la Ligi Kuu ya England mwaka wa 2020. Pia aliiongoza klabu hiyo ya Merseyside kutwaa taji lao la sita la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019.

## Extra Time

# WACHEZAJI 10 BORA WA SOKA WA WAKATI WOTE

**LONDON,** England

MCHEZO maarufu zaidi duniani, mpira wa miguu, umekuwa na mashujaa wa kweli ambao wamevuka mchezo wenyewe na kuweka urithi wao katika akili za mashabiki wa soka milele. Je, inawezekana kuchagua wachezaji bora wa soka wa wakati wote?

**Katika makala haya, tumejaribu kufanya hivyo. Ingawa imekuwa si kazi rahisi, tumejaribu kugawanya uteuzi katika vipengele vitatu: Uwezo wa kushinda mechi, uchezaji wa muda mrefu, na kucheza chini ya presha, twende sasa...**

### #10. Michel Platini

Namba 10 kwenye orodha hii ni Michel Platini. Ufaransa wanaweza kumchukulia mchezaji wao bora kuwahi kutokea ni Zinedine Zidane, lakini kabla ya gwiji huyo wa Real Madrid kufanya uchawi wake, 'Les Bleus' hao walikuwa na mchezaji mwingine mwenye kipaji zaidi ambaye ni Platini.

Akiwa amepewa sifa ya kuifanya Ufaransa kuwa nchi yenye nguvu duniani katika soka, mchezaji huyo alifurahia maisha marefu na yenye manufaa kwa klabu na nchi. Akicheza namba 10, Platini mara zote alionyesha ubora wa hali ya juu kwa kufunga mabao kadhaa muhimu katika maisha yake yote.

Mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or kwa miaka mitatu mfululizo (1983, 84, 85), Mfaransa huyo alifikia kilele cha mchezo wake alipoiongoza Ufaransa kutwaa ubingwa wa Ulaya mwaka 1984 (Euro).

Baada ya kuiongoza Ufaransa kutwaa taji lao la kwanza kubwa la kimataifa na kushinda mataji ya ligi akiwa na Juventus na St Etienne, Platini alistaafu alipokuwa bado kwenye kilele cha kucheza mwaka 1987.

### #9. Johan Cruyff

Hakuna mchezaji na mtu katika historia ya mchezo huu aliyotoa mchango mkubwa zaidi kama Johan Cruyff. Ndiye mwanzilishi wa staili maarufu ya mchezo wa soka ya 'tatal football' kwa Ajax, Barcelona na timu ya Taifa ya Uholanzi.

Mshindi wa Ballon d'Or mara tatu katika maisha yake (1971, 73 na 74), Cruyff aliunda urithi wake kwa mara ya kwanza akiwa Ajax, ambapo aliwaongoza wababe hao wa Uholanzi kutwaa mataji mengi ya ligi na matatu ya Ulaya.

Zaidi ni kwamba, Cruyff anakumbukwa zaidi katika zama za kisasa kwa mabadiliko aliyoleta Barcelona.

Akiwaongoza wababe hao wa Katalunya kutwaa taji lao la kwanza la ligi baada ya miaka 14 mara tu baada ya kujiunga nao. Cruyff anachukuliwa kuwa shujaa na ndiye aliyeanzisha kwa mara ya kwanza staili ya tiki-taka na soka maridadi pale kwenye Uwanja wa Camp Nou.


Cruyff pia alikuwa sehemu ya timu bora zaidi kuwahi kushindwa kutwaa Kombe la Dunia, wakati timu hiyo ya Uholanzi ilipomaliza nafasi ya pili huku Ujerumani Magharibi ikilibeba taji hilo mwaka 1974.

Mwaka 1984 aliiongoza Feyenoord kutwaa taji la ligi, na alikuwa hadithi ya kweli ya mchezo ambaye alikaa katika kiwango cha juu sana kwa miaka 20.

### #8. Ronaldo Nazario

Mchezaji anapoichezea Barcelona, Real Madrid, Inter Milan na AC Milan na bado akiwa hachukiwi, unajua ni kitu cha kipekee. Ronaldo Nazario, ambaye pia anajulikana kama 'Fenomeno' huenda ndiye mshambuliaji wa kiwango cha juu zaidi kuwahi kucheza mchezo huo.

Tangu Ronaldo alipoingia uwanjani kama kijana akiwa na umri wa miaka 17, huko Cruzeiro, hakukuwa na shaka kwamba mshambuliaji huyo wa Brazil alikusudiwa kupata mambo makubwa kwenye mchezo huo. Baada ya kucheza soka la Ulaya akiwa na PSV, Ronaldo huenda alikuwa na msimu wa kipekee zaidi wa maisha yake kule Barcelona, ambapo aliimarisha urithi wake kama moja ya vipaji vikubwa zaidi ambavyo mchezo huwa umewahi kushuhudia.



PELE

Mshindi wa tuzo ya Ballon d'Or mwaka 1997 na 2002, mshambuliaji huyo wa Brazil, labda anakumbukwa zaidi kwa uchezaji wake katika Kombe la Dunia la 1998 na 2002 akiwa na timu ya Taifa ya Brazil.

Mwaka 1998, Ronaldo alikuwa mmoja wa wachezaji bora katika mashindano hayo, akifunga mabao manne kusaidia matatu. Hata hivyo, baada ya kupata degedege saa chache kabla ya mchezo wa fainali, hakuwa katika kiwango bora wakati Brazil ilipofungwa na Ufaransa kwenye fainali.

Mwaka 2002 hadithi ilikuwa tofauti. Akirejea kutoka kwenye jeraha, Ronaldo aliiibuka kuwa mfungaji bora kwenye michuano ya Kombe la Dunia kule Japan na Korea Kusini, akifunga mabao nane na kushinda Kiatu cha Dhahabu.

### #7. Alfredo Di Stefano

Mchezaji bora kabisa wa Real Madrid na sehemu muhimu ya utawala wao katika miaka ya 1950, Alfredo Di Stefano alikuwa na maisha marefu ya miaka 20 ambapo alikuwa miongoni mwa wanasoka bora duniani kwa muda wote.

Di Stefano anayejulikana sana kwa mafanikio yake akiwa na Real Madrid, alifunga mabao 307 katika mechi 396 na kushinda mataji 15 makubwa akiwa na 'Los Blancos' hao, yakiwamo matano mfululizo ya Ulaya.

Akicheza kama mshambuliaji msaidizi au kiungo mkabaji pamoja na Puskas na Gento, Di Stefano alikuwa kwenye kiwango bora kila wakati kwenye mechi kubwa na anashikilia rekodi ya kuwa mchezaji pekee kufunga katika fainali tano za Kombe la Ulaya.

Uchezaji bora wa gwiji huyo wa Real Madrid huenda ulikuja katika ushindi wa 7-3 wa fainali dhidi ya Eintracht Frankfurt, ambapo alitawala mchezo na kudhibiti kila kitu uwanjani.

Watu wengi bado wanamchukulia Di Stefano kuwa mchezaji bora wa Argentina kuwahi kutokea, bora zaidi ya Diego Maradona na Lionel Messi. Mchezaji kamili ambaye angeweza kucheza katika nafasi nyingi kwa urahisi.

Kwa bahati mbaya hakuwahi kupata nafasi ya kucheza Kombe la Dunia.

### #6. Garrincha

Mshindi wa Kombe la Dunia mara mbili na kuchukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji wenye vipaji zaidi kuwahi kutokea, Garrincha alikuwa namba saba kwa Brazil na klabu yake ya Botafogo. Kuanzia mwaka 1953-1965, Garrincha alitumbuiza umma wa Brazili kwa ustadi wake na mbwembwe, mara nyingi akiwaletea watu furaha tele kwa njia ya kipekee aliyocheza soka.

Garrincha alicheza mechi yake ya kwanza ya Kombe la Dunia akiwa na Brazil mwaka 1958 na mara moja akajitambulisha kama mmoja wa wachezaji bora zaidi ulimwenguni, akifunga na kusaidia mabao mengi kwa wachezaji wenzake kama Vava na Pele.

Katika Kombe la Dunia la mwaka 1962, Garrincha aliiongoza Brazil kutokana na kukosekana kwa Pele na alitajwa kuwa mchezaji bora wa mashindano hayo. Wakati mzuri zaidi wa Mbrazil huyo labda ulikuwa katika nusu fainali ya 1962 dhidi ya Chile, wakati alifunga mabao mawili ya kushangaza.

Kwa bahati mbaya, ulevi na majeraha ya Garrincha yalikatisha kipaji chake. Bado, watu wa Brazil watamkumbuka kila wakati gwiji huyo wa miguu yenye matege ya kupinda na uwezo wake wa kufurahisha siku yao kwa jinsi alivyocheza mchezo huo mzuri.

### #5. Zinedine Zidane

Mshindi wa Ballon d'Or mwaka wa 1998, Zidane alikuwa na kazi yenye mafanikio makubwa Juventus na Real Madrid. Hata hivyo, Zidane alikuja kutambulika kwa mara ya kwanza kama mchezaji wa hali ya juu duniani kutokana na uchezaji wake dhidi ya Brazil katika fainali ya Kombe la Dunia mwaka 1998.

Akifunga mabao mawili kwa kichwa katika fainali, Zidane aliipa Ufaransa ushindi wao wa kwanza wa Kombe la Dunia, hivyo kumfanya kuwa shujaa na nyota wa usiku mmoja. Alifuatia kwa uchezaji mzuri katika Euro 2000, ambapo Ufaransa iliishinda Italia na kutawazwa kuwa mchezaji bora wa mashindano.

Baada ya kubadili rekodi ya dunia wakati huo kwenda Real Madrid, Zidane hivi karibuni alionyesha kiwango chake na kuwa mmoja wa wachezaji bora wa safu iliyojaa nyota. Wakati wake maarufu akiwa amevalia jezi nyeupe ulikuja katika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2001-02 dhidi ya Bayer Leverkusen.

Huku matokeo yakiwa 0-0, Zidane alionyesha mbinu ya ajabu ya kukwamisha shuti kali la mguu wa kushoto kutoka nje ya eneo la hatari akiwa hajaliangalia goli. Moja ya mabao mazuri katika historia ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Mfaransa huyo alionyesha kwamba anaweza kutegemewa kila wakati katika hatua muhimu.

Hadi alipostaafu mchezo huo mwaka 2006, Zidane alibakia kuwa miongoni mwa wachezaji bora zaidi duniani. Ukiacha rafu ya kumpiga kichwa mchezaji kwenye fainali ya Kombe la Dunia ya 2006, Mfaransa huyo mashuhuri alikuwa mchezaji aliyefurahi sana akiwa kwenye hatua ya mashindano makubwa.

Kwa maisha yake marefu ya ajabu na uchezaji wake wa ajabu katika fainali ya Kombe la Dunia la 1998, mashindano ya Ulaya 2000 na fainali ya Ligi ya Mabingwa 2002, Zidane anachukuliwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote.

### #4. Cristiano Ronaldo

Mtoto mwenye kipaji cha hali ya juu katika klabu ya Sporting CP, Cristiano Ronaldo aligunduliwa na Sir Alex Ferguson na ni huko Manchester United, ambapo nyota huyo wa Ureno aliimarisha urithi wake kama mmoja wa wachezaji wakubwa wa kizazi hiki.

Azma kali ya kuwa bora, Ronaldo, pamoja na ujasiri na dhamira yake pamoja na kipaji chake cha hali ya juu, imekuwa moja ya majina yanayotambulika katika soka la ulimwengu wa leo.

Ingawa alijipatia umaarufu kama nyota wa Manchester United, ilikuwa ni Real Madrid ambapo aliimarisha hadhi yake ya kuwa mchezaji bora wa muda wote.

Iwe ni kufunga penalti ya mwisho katika mikwaju ya penalti ya mwisho ya Ligi ya Mabingwa au kufunga bao muhimu katika nusu fainali ya Euro 2016, Ronaldo amekuwa akiuonyesha ulimwengu kile anachoweza.

Pamoja na mchezo wake kwa takriban miaka 16 sasa, mshindi huyo wa tuzo ya Ballon d'Or mara tano, aliendelea kuifungia Juventus mabao baada ya kuondoka Madrid na kwenda Turin msimu wa majira ya joto wa 2018.

Kwa sasa, amerejea Manchester majira ya joto yaliyopita. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, hivi majuzi alikuwa mfungaji bora zaidi katika soka la kulipwa (mabao 807) na hat-trick yake dhidi ya Tottenham.

### #3. Lionel Messi

Lionel Messi pamoja na Cristiano Ronaldo, bila shaka ni miongoni mwa wachezaji wakubwa zaidi wa kizazi hiki. Akiwa ameonekana kama mtoto mpya wa La Masia mwaka wa 2005, Messi, kwanza chini ya ulezi wa Frank Rijkaard na kisha, muhimu zaidi, chini ya Pep Guardiola, alijidhihirisha kuwa mmoja wa wachezaji wakubwa waliowahi kupamba mchezo huo.

Wakati Messi amefunga katika kila aina ya mechi muhimu za klabu - fainali za Ligi ya Mabingwa, nusu fainali, Fainali za Copa del Rey (Kombe la Mfalme), Clasicos dhidi ya Real Madrid, alikuwa na shida wakati akiichezea Argentina.

Baada ya kupoteza fainali tatu mfululizo akiwa na timu ya taifa, Messi alistaafu kuichezea timu ya taifa kwa muda mfupi, kisha akarejea miezi miwili baadaye na hatimaye alimaliza ukame wake na Argentina kwa kunyanyua Copa America mwaka 2021.

Haijalishi atafanya nini kuanzia sasa, Messi atazingatiwa kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote. Mchezaji pekee aliyeshinda Ballon d'Or mara saba, mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina, aliondoka Barcelona majira ya kiangazi mwaka jana katika uhamisho wa kushtukiza na kujiunga na PSG.

### #2. Diego Maradona

Diego Maradona kama mchezaji na mtu anayekumbukwa zaidi katika mechi dhidi ya Uingereza kwenye Kombe la Dunia la 1986. Nyota huyo wa Argentina, alichachafya safu ya ulinzi ya Uingereza na kufunga mabao makubwa zaidi ya wakati wote.

Akiwa na kipaji cha hali ya juu, Maradona angeweza kufanya mambo na mpira wa miguu ambao wanadamu hawakuweza hata kuota. El Diego alikuwa nyota wa ushindi maarufu wa Argentina wa Kombe la Dunia mwaka 1986.

Maradona pia alifanya yake kwenye kazi ya Klabu Ulaya, kwanza Barcelona na kisha Napoli. Ingawa mchezaji huyo mashuhuri alishinda tu Copa del Rey na Supercopa Espana wakati alipokuwa Barcelona.

Akiwa Napoli, Maradona alishinda mataji mawili ya Serie A. Hadi leo Maradona bado ni mwana kipenzi wa Napoli na anachukuliwa kuwa mchezaji bora zaidi kuwahi kucheza Ulaya. Maradona aliaga dunia mwaka 2020 kutokana na mshtuko wa moyo.

### #1. Pele

Gwiji wa Brazil, Pele anachukuliwa kuwa mwanasoka bora zaidi wa wakati wote. Hakuna mchezaji aliyeshinda Kombe la Dunia zaidi yake, na hiyo pekee inapaswa kutosha kuhalalisha kujumuishwa kwa Mbrazil huyo katika kilele cha orodha hii.


Mfungaji bora zaidi, Pele pia alikuwa kitovu cha ushambuliaji kwa klabu na nchi. Takwimu zake za mabao ni za kushangaza; ndiye mchezaji pekee aliyefunga zaidi ya mabao 1200.

Mchezaji mdogo zaidi kuwahi kutokea (miaka 17 na siku 249) kufunga katika Kombe la Dunia. Pele alifunga mara mbili katika fainali ya Kombe la Dunia 1958 dhidi ya Uswisi.

Ingawa aliweza kucheza mechi moja pekee katika Kombe la Dunia la mwaka 1962 kwa sababu ya jeraha, ilikuwa mwaka 1970 ambapo aliimarisha urithi wake kama mchezaji bora zaidi wa wakati wote. Wakicheza kandanda maridadi, Brazil ilitawala mashindano hayo, huku Pele akishinda tuzo ya Mpira wa Dhahabu na Mchezaji Bora.

## Nukuu

"Ninajijumuisha katika hilo. Tulichofanya leo (juzi), nilichokifanya leo (juzi), hakikutosha kuwa kwenye jezi ya Man United na ninakubali," **Kiungo wa Manchester United, Bruno Fernandez baada ya kuangukia pua ya mabao 4-0 dhidi ya Brighton and Hove Albion kwenye Uwanja wa Amex juzi.**



"Kwa kweli, nimechoka sana. Nimechoka sana baada ya mchezo huu (dhidi ya Liverpool juzi). Huu ulikuwa ni mchezo mgumu zaidi ambao nimewahi kukutana nao. Hatua ni nzuri kila wakati pale Anfield, ni wazi kuwa ni mahali pagumu na kufanya kazi kwa bidii kumezaa matunda," **Nyota wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min akikiri ugumu aliokutana nao kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Liverpool juzi.**



"Nataka kucheza na Madrid(fainali Ligi ya Mabingwa Ulaya), lazima niseme ukweli, kwa sababu tulipoteza katika fainali dhidi yao, nataka kucheza dhidi yao, na ninatumaini kushinda dhidi yao pia," **mshambuliaji wa Liverpool Mohamed Salah, ambaye hadi sasa msimu huu amehusika katika mabao 45 kwenye michuano yote (mabao 30, asisti 15).**



# MABAO 10 BORA ZAIDI RAUNDI YA 22 LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

ILITEGEMEWA kabisa na wataalamu wa soka kuwa kwenye mechi za mwisho za Ligi Kuu, timu zitafunguka na kufungana mabao mengi.

**Ni kwa sababu timu sasa zinahitaji ushindi zaidi kuliko sare, kwa sababu mbali na kuwa na timu zinazosaka ubingwa, lakini baadhi ya timu zinaisaka nafasi ya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao.**

Msimu huu pia ni kwamba timu nyingi zinatafuta pointi tatu kwa udi na uvumba ili zikae kwenye nafasi nzuri ya kutoshuka daraja. Ni msimu ambao kumekuwa na timu nyingi zikijitahidi zaidi kubaki Ligi Kuu. Hakuna timu yenye uhakika wa kubaki kwa timu 14 kati ya 16 zinazoshiriki.

Ndiyo maana mechi nyingi sasa zimekuwa na mabao mengi kwa sababu timu zinafunguka.

Tumeona wachezaji kadhaa wakifunga mabao mazuri kwenye baadhi ya mechi za raundi ya 21 na 22 kwa ajili ya kuzisaidia timu zao.

Haya ni mabao makali yaliyofungwa raundi ya 21 na 22 kwenye mechi za Ligi Kuu...


**#1. George Mpole (Geita Gold vs Azam)**

Straika huyu ambaye kwa sasa ameshafikisha mabao 12 sawa na Fiston Mayele wa Yanga, alipiga bao kali kwenye mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya timu yake ya Geita Gold na Azam FC, mchezo uliochezwa Aprili 29, mwaka huu kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu, Geita.

Alipata pasi akiwa mita 30. Hakuwa na mambo mengi, alitisha kama anataka kutoa pasi, mabeki wa Azam wakadanganyika, akaachia shuti kali la chini chini lililojaa wavuni dakika ya 26 ya mchezo, likiwa ni la kwanza kwenye mechi hiyo, iliyoisha kwa sare ya mabao 2-2.

**#2. Jumanne El Fadhili (Prisons vs Polisi Tanzania)**

Kazi nzuri iliyofanywa na straika wa Prisons, Jeremiah Juma kupiga faulo ya mbali, ukatemwa na kipa wa Polisi Tanzania, Metacha Mnata, ulimkuta Jumanne El Fadhili akiwa kwenye nafasi nzuri, akijitenga na wachezaji wengine, akaukwamisha wavuni dakika ya 16 ya mchezo na kuwa bao pekee kwenye mechi hiyo, Prisons ikishinda bao 1-0. Ilikuwa ni Mei Mosi, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya.




Beki wa Simba, Shomari Kapombe, mmoja wa wachezaji waliofunga mabao makali kwenye mechi za raundi ya 21 na 22 ya Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: MAKTABA**

**#3. Shomari Kapombe (Simba vs Namungo)**

Alipenyezewa mpira na Mzamiru Yassin baada ya msako wa nguvu, Simba ikitafuta bao la kusawazisha.

Kapombe aliwakwepa mabeki wawili wa Namungo na kukaa mbele ya mpira, kabla ya kuukwamisha wavuni dakika ya 41 ya mchezo, mechi ikichezwa Mei 3 kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2.

**#4. Nzigamasabo Steve (Biashara United va Mtibwa Sugar)**

Ulikuwa mpira mrefu kutoka kwenye winga ya kulia ukionekana hauna madhara, lakini raia huyo wa Burundi akitumia uzembe wa mabeki wa Mtibwa wakidhani mpira ungeisha muda wowote, kuruka juu akiwa amezungukwa na wachezaji wa timu pinzani akaijaza wavuni, dakika tatu za nyongeza na kusawazisha bao na kuwa 1-1, kwenye Uwanja wa Nyamagana, Mwanza. Mei 2, mwaka huu.

**#5. Jacob Massawe (Namungo vs Simba)**

Shiza Kichuya, mchezaji wa zamani wa Simba, alipiga kona dakika ya saba ya mchezo kati ya timu ya Namungo na waajiri wake wa zamani. Ilulu mjini Lindi.

Massawe hakuruka juu, ila alitumia uzembe wa mabeki wa Simba kuusubiri ufike golini, yeye aliukimbilia kama anayekwenda kuupokea, akapiga kichwa kwa kuugeuza na ukajaa wavuni Mei 3, mechi iliyoisha kwa sare ya mabao 2-2.

**#6. Ismail Aziz (Azam vs Geita Gold)**

Kazi nzuri iliyofanywa na Charles Zulu kuambaa na mpira na kupiga krosi shuti, ukaleta kizaazaa langoni, kabla ya kumfikia Aziz aliyekuwa anafuatilia nyendo za mpira huo, akaukwamisha wavuni dakika ya 35, mechi ilichezwa Aprili 29, mwaka huu Uwanja wa Shule ya Sekondari, Nyankumbu, Geita na kumalizika kwa sare ya mabao 2-2.

**#7. Obrey Chirwa (Namungo vs Simba)**

Uzembe mwingine tena wa mabeki wa Simba wa mipira iliyokufa ilimfanya Obrey Chirwa apachike bao maridadi kwenye Uwanja wa Ilulu mjini Lindi, Mei 3, iliyoisha kwa sare ya mabao 2-2.

Ni kona nyingine iliyochongwa na Kichuya, safari hii haikuguswa na mchezaji yeyote na kwenda pembeni mwa uwanja. Reliants Lusajo akaukimbilia na kuuzuia, na akiwa kwenye kona hiyo alimimina krosi, mfungaji akaruka mbele ya Joash Onyango na Mohamed Hussein 'Tshabalala', akaujaza wavuni dakika ya 54.

**#8. Danny Lyanga (Geita Gold vs Azam)**

Lyanga alifunga bao maridadi, akiutokea ghafla mpira ambao haukuwa wake. Uliingizwa mpira kwenye nje ya eneo la hatari na wachezaji wa Geita Gold wakawa wanapasiana. Mabeki wa Azam hawakumtia kwenye hesabu za kumkaba mfungaji. Pasi ilipigwa kwa mtu mwingine, yeye akautokea ghafla na kuachia shuti lililojaa wavuni dakika ya 81, bao la pili kwenye Uwanja wa Nyankumbu, Aprili 29, ikiisha kwa sare ya mabao 2-2.

**#9. David Luhende (Kagera Sugar vs Azam)**

Mei 3, mwaka huu kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, dakika ya 54, Luhende alifumua shuti kali kwenye mpira wa faulo uliokwenda moja kwa moja wavuni na kuipa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Azam FC. Ni mmoja kati ya mabeki wachache nchini wenye uwezo wa kufunga mipira ya faulo, na mabao yake mengi hufunga kwa staili hiyo.

**#10. Kibu Denis (Namugo vs Simba)**

Yalikuwa ni kama mashindano ya kupiga vichwa baina ya wachezaji wa Simba dhidi ya Namunngo. Ilikuwa kwenye eneo la hatari la Namungo. Mtu wa kwanza kuugusa kwa mguu ni Kibu, ulitua kwenye goti na kupiga mpira uliokwenda wavuni kulia kwa kipa dakika ya 79, likiwa ni la kusawazisha timu zikitoka sare ya mabao 2-2, Uwanja wa Ilulu mjini Lindi.

**JE, WAJUA?**



WAKATI zikiwa zimebaki raundi tatu kabla ya Ligi Kuu England kufikia ukingoni msimu huu wa 2022/23 huku Liverpool ikiwa kileleni kwa pointi 83 (kabla ya Man City kucheza mechi yake ya 35 jana). Kama City yenye alama 83 itashinda mechi zake zote zilizobaki kuanzia ya jana, itakuwa timu pekee kwenye ligi hiyo, itakayofikia rekodi ya kumaliza msimu na pointi nyingi zaidi iliyowekwa na Chelsea msimu wa 2004/05 baada ya kuuhitimisha na pointi 95.





# Watumishi Chemba kortini madai kuisababishia serikali hasara mil.85/-

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATUMISHI wa tatu wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya hiyo kwa tuhuma za kuisababishia serikali hasara ya Sh. milioni 85.5, kutokana na udanganyifu wa malipo waliofanya kwa M-mkandarasi Mrimi International (T) Co. LTD.

Watumishi hao wanakabiliwa na tuhuma za kugushi nyaraka za kumdanganya mwajiri wao kulipa malipo kwa mkandarasi huyo aliyekuwa akijenga miundombinu ya maji kwenye vijiji vya Lahoda-Kisande vilivyopo wilayani humo kwa mkataba wa Sh. milioni 451.39.

Akitoa maelezo ya shauri la uhujumu uchumi namba nne la mwaka 2022 mwishoni mwa wiki mbele ya Hakimu wa Mahakama hiyo, Ester Mwakalinga, Mwanasheria wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Leonard Haule, alidai ndani ya mkataba huo mkandarasi huyo alilipwa fedha kiasi hicho (milioni 85.5) kwenye kazi ambazo hazikufanyika kinyume na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Alidai watuhumiwa hao wanakabiliwa na mashtaka manne, ambapo matatu ni matumizi ya nyaraka kumdanganya mwajiri kinyume na kifungu cha 22 cha Sheria hiyo na shtaka la nne ni kuisababishia serikali hasara hiyo. "Watuhumiwa wanadaiwa kutenda kosa hilo kati ya Oktoba 2014 na Mei, 2016 ambapo walidanganya kuwa mkandarasi Mrimi International(T) Co. LTD ambaye alipewa kazi ya kujenga miundombinu ya maji katika vijiji vya Lahoda-Kisande vilivyopo wilayani Chemba kwa mkataba wa Sh.451,399,000, alifanya kazi na kustahili kulipwa malipo kwa kiasi ambacho ni zaidi ya kazi halisi iliyofanyika na kusababisha hasara husika,"alidai.

Aliwataja waliofikishwa mahakamani kuwa ni aliyekuwa Kaimu Mhandisi wa Wilaya hiyo, Rodrick Mbepera, Fundi Sanifu wa Maji, Lyimo Yusuph, na Wallace Daffa ambaye ni Fundi Sanifu Mwandamizi.

Alisema pia Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Mrimi International (T) Co. LTD, Paulo Mrimi, pia amefikishwa mahakamani hapo.

Hata hivyo, washtakiwa hao walikana mashtaka dhidi yao na kuachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti ya dhamana waliyopewa na mahakama na kesi hiyo itatajwa tena Mei 13, mwaka huu.



Muuza mboga katika soko la Mbezi Mwisho Manispaa ya Ubungo jijini Dar es Salaam akiwa amejipumzisha kwenye biashara yake huku wenzake wakisubiri wateja juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Kongamano kujadili matatizo ya ushirika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), imeandaa kongamano la pili la masuala ya utafiti kwenye sekta ya ushirika ili kutatua kero zilizopo kwenye sekta hiyo kupitia utafiti.

Kongamano hilo linatarajiwa kufunguliwa na Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde na litafanyika kwa siku tatu kuanzia Mei 11 hadi 13, mwaka huu, jijini Dodoma.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume hiyo, Dk. Benson Ndiege alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa.

Alisema kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) wameandaa kongamano hilo ili kutatua kero zilizopo kupitia tafiti zilizofanyika na uzoefu wa wadau mbalimbali.

"Kongamano linalenga kutoa fursa kwa watafiti pamoja na wadau wengine wa sekta ya ushirika kukutana na wanachama, viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika, ili kujadiliana matokeo ya utafiti na utatuzi wa changamoto zilizopo katika sekta hii,"alisema.

Mrajis huyo alisema tafiti mbalimbali zinazohusu sekta ya ushirika zimekuwa zikifanywa na wadau mbalimbali vikiwamo vyuo vya elimu ya juu, mashirika yasiyokuwa ya kiserikali, wadau wa ushirika na wengine.

"Tafiti hizi zimekuwa zikitoa mapendekezo ya utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazokabili maendeleo ya ushirika nchini, tumewalenga wanachama, viongozi na watendaji wa vyama vya ushirika kwa kuwa wamekuwa hawapati fursa ya kupata matokeo ya tafiti hizi na mapendekezo yake," alisema.

# Wenye ulemavu wasaidiwa bima za afya

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

TAASISI ya Foundationi for Disabilities Hope imetoa msaada wa bima za afya kwa watu wenye ulemavu 96, wakiwamo wanafunzi wa shule za msingi na sekondari za mkoani Dodoma.

Ofisa Habari wa taasisi hiyo, Bertha Nswebe, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akitoa taarifa fupi katika hafla ya kukabidhi bima hizo jijini hapa.

Alisema hadi sasa wamewafikiwa watu wenye ulemavu 194, kwa kuwapatia bima za afya.

"Na katika malengo yetu kwa mwaka huu ni kufikia kaya za watu wenye ulemavu 300 ambapo wanufaika wake tunategemea watakuwa ni watu wenye ulemavu zaidi ya 1,800 ambao watanufaika na mpango wa bima za afya za CHF."

"Aidha katika mpango wa utoaji wa bia za afya tunategemea pia kuwapatia bima za afya za NHIF watoto 200," alisema. Kadhalika, alisema kutokana na kundi la watu wenye ulemavu kukumbwa na kikwazo kikubwa cha kiuchumi hali inayosababisha kushindwa kumudu gharama za matibabu pindi wanapougua maradhi mbalimbali. Alisema kwa kutambua hali hiyo taasisi hiyo iliona ni vyema kuwawezesha watu wenye ulemavu kupata bima ya afya ili kuwapunguzia gharama za matibabu na kutoa uhakika wa matibabu kwa wakati bila kuwa na kikwazo cha fedha.

"Katika kutekeleza mpango huu wa utoaji wa bia za afya kwa watu wenye ulemavu yapo mafanikio ambayo mpaka sasa tumeshayafikia. Tumefanikiwa kuwafikia watu wenye ulemavu 430 kwenye zoezi la ubainishaji na kati yao mpaka sasa tumefanikiwa kuwapatia bima za afya watu 194," alisema.

Akilabidhi bima hizo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabiri Shekimweri, aliwataka watu ulemavu kujitokeza kwa wingi kushiriki kwenye Sensa ya Watu na Makazi Agosti 23, mwaka huu.

Alisema Agosti 23, mwaka huu serikali inakwenda kutekeleza Sensa ya Watu na Makazi hivyo ni lazima kwa kila mtu wenye ulemavu kujitokeza ili kuhesabiwa.

"Mwaka huu serikali inakwenda kutekeleza zoezi la sensa ya watu na makazi kikamilifu kwa kuhesabu watu pamoja na makazi hivyo mjitokeze wote kuhesabiwa kwani usipohesabiwa share yako haitakuwapo mkijitokeza mtaisaidia kupata takwimu sahihi na kuweza kuwasaidia,"alisema Shekimweri.

Aidha, aliwataka watu wenye ulemavu kuchangamkia fursa ambazo zinatolewa na serikali ili kujikwamua kiuchumi badala ya kuendelea kuwa tegemezi. "Jiji la Dodoma linajitahidi sana kutenga asilimia 10 ya mapato yake kwa ajili ya kuwezesha makundi ya vijana, wanawake na walemavu lakini walemavu bado mwamko wao katika kukopa uko chini sana,"alisema.





## W'biashara waonywa bima za COMESA

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAFANYABIASHARA waliopo kwenye mpaka kati wa Tanzania na Malawi uliopo Kasumulu wilayani Kyela wametahadharishwa kuacha kujihusisha na uzalishaji wa bima feki za Soko la Pamoja na nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika (COMESA) kuwa watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Mkurugenzi wa Masoko wa Shirika la Bima la Taifa (NIC), Yesaya Mwakifulefule, alitoa tahadhari hiyo juzi wakati maofisa wa shirika hilo waliposhirikiana na vyombo vya dola kukagua stika za bima zinazouzwa na wafanyabiashara kwenye mpaka huo.

Alisema wamekuwa wakipokea malalamiko ya mara kwa mara kutoka kwa wateja kuwa wamekuwa wakiuziwa bima feki katika eneo hilo hali ambayo imekuwa ikiwasababishia vikwazo mbalimbali kwenye shughuli zao.

Alisema uuzwaji huo wa bima feki umekuwa ukiisababishia serikali hasara kila mwaka kutokana na kutopata fedha halali baada ya wahuni hao kuuza stika hizo na kwamba biashara hiyo inasababisha stika halali kutouzwa.

"Stika hizi zimekuwa zikitumika pia katika mpaka wa Tunduma, sasa tumeamua kuja kufanya operesheni hii ili kukomesha vitendo hivi haramu na kuondoa upotevu huu wa mapato ya serikali," alisema Mwakifulefule.

Meneja wa NIC Mkoa wa Mbeya, Jastin Seni, alisema katika operesheni hiyo waliwakamata vijana kadhaa na kuwapeleka kwenye vituo vya polisi kwa ajili ya uchunguzi zaidi kabla ya kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kupelekwa mahakamani.

Aliwataka vijana wa maeneo hayo ya mpakani kuacha tabia hiyo ya kuuza stika feki akisisitiza kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria na inaingia kwenye makosa ya uhujumu uchumi.

Alisema ili kuongeza ufanisi wa udhibiti wa biashara hiyo wanakusudia kufungua ofisi ndogo katika mpaka wa Kasumulu ili kuwarahisishia wateja.

# Vijiji 31 Mbarali vyabaki Hifadhi Ruaha

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI imeridhia vijiji 31 kati ya 58 vya Wilaya ya Mbarali vilivyoko ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Ruaha kutoondolewa na badala yake wananchi waendelee kufanya shughuli zao za maendeleo bila kuathiri mazingira.

Aidha, imesema inaendelea kufanya tathmini vijiji vingine 27 vilivyobakia kwa ajili ya kuangalia athari za kimazingira kabla ya kuamua kuviondoa ndani ya hifadhi ama kuvibakiza.

Vijiji hivyo ni vile ambavyo vilibainika kuwa ndani ya hifadhi hiyo baada ya Tangazo la Serikali namba 28 (GN.28) la mwaka 2008 ambalo lilikuwa linaashiria kuipanua hifadhi hiyo na hivyo kuzua mgogoro kati ya wananchi na serikali.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawaziri watano wa Kisekta, Angelina Mabula ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alitangaza uamuzi huo juzi jijini Mbeya wakati wa kikao maalumu cha kamati hiyo, maofisa wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya.

Alisema vijiji 27 vilivyobakia endapo wananchi watatakiwa kulipwa fidia watalipwa na watakaotakiwa kuondoka bila kulipwa fidia wataondolewa kwa utaratibu ili kuepusha migogoro mingine kuibuka baina yao na serikali.

Alisema kuna baadhi ya maeneo uharibifu wa mazingira ni mkubwa kutokana na wingi wa mifugo usioendana na eneo husika na kwamba ndiyo maana imekuwa ikiibuka migogoro ya mara kwa mara kati ya wananchi hao na hifadhi.

"Kuna eneo unaambiwa lilitakiwa mifugo isizidi 65,000 lakini mpaka sasa mifugo iliyopo ni zaidi ya 260,000, sasa tunaendelea na tathmini ili kujua ukubwa wa tatizo, lakini kwa hivi vijiji 31 Rais Samia Suluhu Hassan amesema visiguswe kabisa," alisema Mabula.

Alisema ili kupunguza matatizo ya kimazingira, wafugaji wanatakiwa kupewa elimu ili waondokane na ufugaji wa kienyeji na badala yake wafuge kisasa na wakulima waachane na kilimo cha mazoea walime kisasa. Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema wahifadhi wamekuwa wakiuawa na wananchi mara kwa mara huku wakitetewa na wanasiasa jambo ambalo alisema sio zuri kutokana na kwamba wahifadhi hao wanafanya kazi yenye manufaa kwa taifa.

Alisema mara nyingi wananchi wakidhurika kutokana na shughuli za kiuhifadhi wamekuwa wakitetewa na wanasiasa lakini inapotokea mhifadhi akaumizwa ama kuuawa na wananchi hakuna wa kumtetea.

Alisema hivi karibuni wamezika wahifadhi kadhaa waliouawa na wananchi kwenye maeneo tofauti tofauti lakini hakuna mwanasiasa aliyeinuka na kukemea vitendo hivyo vya wananchi.

"Nimesikia kwamba Mkuu wa Wilaya ana maisha magumu kutokana na migogoro hii, naomba tuwaingize na wahifadhi kwenye kundi hilo, hakuna watu wana maisha magumu kama wahifadhi, tunazika kila siku wanaouawa na wananchi," alisema Masanja.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliwataka viongozi wa Mkoa wa Mbeya, kusaidia kulinda vyanzo vya maji vya Mto Ruaha ambao ni miongoni mwa vyanzo muhimu vya maji ya kutumia binadamu na wanyama pamoja na uzalishaji wa umeme.

Alisema Bwawa la Mwalimu Nyerere ambalo linajengwa na serikali linategemea maji ya Mto Ruaha na kwamba hata viumbe hai vilivyomo ndani ya Hifadhi ya Mto Ruaha vinategemea maji hayo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliwataka wadau wote wa kushirikiana kulinda mazingira kwa maelezo kuwa athari za kimazingira zinaathiri makundi yote wakiwamo wakulima na wafugaji.




Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundu (katikati), akishirikiana na Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, kukata utepe kuzindua wimbo maalumu wa kutoa elimu ya kukabiliana na magonjwa ya zinaa ulioandaliwa na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Loleza. Kushoto ni Mtafiti kutoka NIMRI, Dk. Ruby Mcharo na kulia ni Mkuu wa Shule hiyo, Ibrahim Ngao. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wanafunzi 40% hawana uelewa magonjwa ya zinaa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

ASILIMIA 30 ya wanafunzi wa vyuo na sekondari nchini hawana uelewa kuhusu magonjwa ya zinaa kutokana na kuwa na elimu ndogo kuhusu magonjwa hayo hali ambayo inawaweka katika mazingira hatari ya kupata magonjwa hayo.

Hali hiyo imebainika kufuatia utafiti maalumu uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMRI) katika taasisi mbalimbali za elimu mkoani Mbeya ambapo inaelezwa kuwa magonjwa hayo ni hatari kwa afya za vijana.

Mtafiti kutoka katika taasisi hiyo, Dk. Ruby Mcharo, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa uzinduzi wa wimbo maalumu wa kuhamasisha vijana kujikinga na magonjwa hayo ulioandaliwa na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Loleza jijini Mbeya.

Alisema utafiti huo ulibaini kuwa asilimia 70 ya wanafunzi wenye elimu ya magonjwa ya zinaa wanaipata wakiwa katika shule za sekondari lakini, uelewa wao bado unakuwa uko chini hali ambayo inawafanya bado waendelee kupata madhara.

Alisema kutokana na tatizo hilo waliamua kuanzisha programu maalumu ya kutafuta mbinu bora za kufikisha elimu kwa vijana kwa kuwashirikisha wao wenyewe kubuni mbinu hizo.

Alisema awali wanafunzi walitunga maigizo mbalimbali yanayoelimisha kuhusu magonjwa hayo lakini baadaye walibaini kuwa ufanisi wake ni mdogo na hivyo wakaamua kutumia sanaa ya kuimba chini ya usimamizi wa watafiti.

"Tuliwashirikisha wanafunzi kwa kujaza madodoso maalumu na tukabaini wengi uelewa wao ni mdogo, baadhi walikuwa hawajui kabisa dalili za magonjwa haya na kwa kiwango kikubwa magonjwa haya ni hatari na yanaweza kuwasababishia matatizo watakapofikia umri wa kuzaa," alisema Dk. Ruby.

Aliiomba serikali kuutumia wimbo uliotungwa na wanafunzi hao wa Loleza Sekondari kwenye mitaala ya elimu ili wanafunzi wengi zaidi wapate elimu na kuwa na uelewa mpana juu ya magonjwa hayo.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Loleza, Mwalimu Ibrahim Ngao, alisema moja kati ya matatizo yanayowakabili watafiti wakiwamo watafiti hao wa magonjwa ya binadamu ni kukosa ushirikiano kutoka kwa wadau wanaohusika.

Alisema utafiti uliofanywa na wataalamu kutoka NIMRI ni muhimu kwa taifa kutokana na kwamba unasaidia kujua ukubwa wa tatizo na namna ya kuanza kukabiliana nalo. "Nawashukuru sana NIMRI kwa kuchagua shule yetu kwa ajili ya kazi hii muhimu, na sisi tuliwapa ushirikiano kwa sababu tunajua umuhimu wa utafiti, niwaombe wasomi wengine wasiwe wanabana taarifa wanazozihitaji watafiti," alisema Mwalimu Ngao.

Baadhi ya wanafunzi waliotunga wimbo huo walisema walitunga wimbo huo na kuurekodi ili usambae na kuifikia jamii kubwa ya Watanzania na hata nje ya nchi.

Mmoja wa wanafunzi hao, Catherine Majibele alisema wimbo huo una maudhui ambayo yanalenga kuwaelimisha vijana kuhusu namna magonjwa ya zinaa yanavyoambukizwa, athari zake pamoja na namna ya kujikinga. Akizindua wimbo huo, Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, aliwataka mabinti kuacha kujiingiza kwenye zinaa kabla ya kutimiza ndoto zao akisisitiza kuwa magonjwa ya zinaa yanaathiri nguvu kazi ya taifa.

Alisema ili wanafunzi wakabiliane vizuri na magonjwa hayo wanatakiwa kushiriki vizuri kwenye ratiba za shule ikiwamo ratiba ya michezo ili wasiwe na mawazo ya kwenda kufanya zinaa.

Alisema yeye atashiriki kuusambaza wimbo huo katika maeneo mbalimbali ikiwamo kwenye redio za kijamii na bungeni ili uwafikie wanafunzi wote nchini huku akiwasihi wazazi kuongea na watoto wao kuhusu masuala ya zinaa bila kuwaficha.





Wafanyakazi Zanzibar wakishangilia hotuba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wakati akiwahutubia katika kilele cha kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani iliyofanyika jana katika viwanja vya Maisara Suleiman. **PICHA: IKULU**

# Mwinyi kuongoza dua ya mwanazuoni

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anatarajiwa kuongoza dua maalum ya kumbukumbu ya karne moja tokeo kufariki kwa mwanazuoni maarufu Afrika ya Mashariki na kati Sheikh Al-habib Sayyid Ahmad bin Sumait, ambaye alikuwa kadhi mkuu wa Zanzibar aliyefariki mwaka 1925.

Dua hiyo ambayo itafanyika Mjini Zanzibar Mei 13, mwaka huu, itahudhuriwa na zaidi ya wanazuoni 38 ikiwamo makadhi wakuu pamoja na Mufti wakuu kutoka nchi tano.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Mjini Zanzibar Msimamizi wa Mkuu wa shughuli hiyo, Sheikh Mohamed Omar Alsheikh, alisema tukio hilo linatarajiwa kuhudhuriwa na wanazuoni kutoka katika nchi za Comoro, Kenya, Yemen, Umoja wa Falme za Kiarabu, na Uingereza.

Aliwataja baadhi ya viongozi wa ngazi za juu za kidini watakaohudhuria ni Mufti Mkuu kutoka Comoro Sheikh Abubakar Abdalla Jamalullayl pamoja na Kadhi Mkuu wa nchi hiyo, Sheikh Muhammed bin Othman.

Alieleza kuwa tukio hilo la kumbukumbu ya mwanazuoni huyo linatarajiwa kuanza wiki ijayo Mei 13 hadi 16 kwa kuanza kwa kisomo cha Maulid (hauli) itakayofanyika katika Msikiti wa Ijumaa wa Malindi.

Aidha, alisema ujumbe wa wanazuoni hao unatarajiwa kuonana na viongozi wengine wa kitaifa pamoja na kuhudhuria mihadhara mbalimbali ya kidini, na kwamba jambo hilo ni bahati kwa Zanzibar.

Sheikh Subeit ambaye anatimiza miaka 100 tokea kufariki aliwahi kuwa Kadhi Mkuu wa Zanzibar katika kipindi cha utawala wa Sultani Barghashi bin Said katika mwaka 1883 akiwa na umri wa miaka 22, na kwamba ilipofika mwaka 1886 aliacha kazi na kwenda nje kwa masomo.

Mwaka 1888 baada ya kurudi masomoni aliendelea na wadhifa wake wa Kadhi Mkuu wa Zanzibar chini ya utawala wa Sultani Khalifa bin Said hadi ilipofika mwaka 1925.

# Zanzibar yajipanga kukuza utalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imedhamiria kuiendeleza sekta ya utalii na kuongeza thamani na ubora, ili kuendelea kukuza uchumi wa nchi.

Hayo yalielezwa na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah wakati akisoma hotuba kwa niaba ya Rais Husein Ali Mwinyi kwenye hafla ya uzinduzi wa mchango wa utalii katika pato la taifa Zanzibar, iliyofanyika ukumbi wa Golden Tulip Uwanja wa ndege Zanzibar.

Alisema serikali ina jukumu la kuendeleza vivutio vya kitalii hasa kupitia uchumi wa buluu ambapo rasilimali za bahari zitatumika ipasavyo kwa ajili ya kuendeleza sekta hiyo ikijumuisha ujenzi wa hoteli na migahawa.

"Msisitizo mkubwa wa serikali ni kuendeleza uchumi wa buluu hii itajumuisha ujenzi wa hoteli na migahawa na tutatumia fukwe na bahari kwa ajili ya michezo ya utalii kama vile soka za ufukweni na resi za ngalawa," alisema.

Aidha, alisema kuwa uzinduzi wa zana hiyo inaonyesha wazi jinsi serikali ya Zanzibar inavyothamini na kuiendeleza sekta ya utalii kwa kuwa ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Zanzibar.

Alisema uwepo wa utoaji wa takwimu sahihi katika sekta mbalimbali za kiuchumi itasaidia kufikia malengo serikali imejiwekea ili kuendana na maendeleo endelevu.

Kwa mujibu wa Abdullah, nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara bado tatizo la utoaji wa takwimu sahihi jambo ambalo linasababisha kuzorotaji kwa maendeleo kwenye sekta mbalimbali.

Aliitaka Kamisheni ya Utalii na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu na taasisi nyingine kuendeleza tafiti katika utengenezaji wa mifumo kwa lengo la kupata mchango halisi wa utalii Zanzibar.

Aidha, alisema serikali imejipanga kuhakikisha inaziwezesha taasisi husika, ili kuhakikisha mahitaji ya uendelezaji wa mfumo huo yanapatikana kwa wakati.

Naye Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said, alisema mfumo huo ulianzishwa na Shirika la Utalii Duniani kwa lengo la kupata takwimu sahihi za kitalii ili kusaidia kupima pato la utalii.

Alisema kuwa kazi kubwa ya zana hiyo ni kuchambua kwa undani nyanja zote za mahitaji ya utalii ikiwamo bidhaa na huduma zinazohusiana na shughuli za wageni.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Rahim Bhaloo, alieleza kuwa zana hiyo itasaidia kuzalisha ajira kwa wananchi na wawekezaji na kupelekea serikali kufikia malengo iliyojipangia.

# Mnazi Mmoja sasa yaelemewa wajawazito

**Na Mwandishi Wetu**

MKE wa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Zainab Kombo Shaib, amewataka wajawazito kuvitumia vituo vya afya kujifungua, ili kupunguza msongamano katika Hospitali ya Rufani Mnazi Mmoja.

Zainab aliyasema hayo alipotembelea kuona hali halisi na kwajulia hali mama wajawazito na waliojifungua waliolazwa katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Mjini Zanzibar.

Alisema aliona katika wodi hiyo wagonjwa waliolazwa na kujifungua kwa njia ya kawaida au upasuaji kitanda kimoja kikitumiwa na mgonjwa kati ya mmoja hadi watatu jambo linalohatarisha afya zao.

Kwa mujibu wa Zainab, upungufu wa vitanda na idadi ya wajawazito ni kubwa jambo linalosababisha msongamano, na kwamba ni muhimu kutumia vituo vya afya kupata huduma kuliko kila mmoja kuenda Mnazi Mmoja.

Alisema ni muhimu wagonjwa wanaokwenda hospitalini humo wawe ni wenye matatizo makubwa yanayohitaji utaalam wa juu zaidi, ili kupunguza athari zinazoweza kuletwa na msongamano.

Aidha, serikali inatambua changamoto zilizopo sekta ya afya na kwamba jitihada zimeongezwa kuboresha, ili wananchi wapate huduama bora za afya.

Kwa upande wake, msimamizi wa wodi hiyo, Dk. Magreti Selvesta, alisema pamoja na mrundikano wa wagonjwa pia kuna uhaba wa vifaa tiba kwa wagonjwa wa dharura wanaotakiwa kufanyiwa upasuaji.

Jingine ni uhaba wa wafanyakazi na kwamba kwa mujibu wa taratibu mkunga mmoja anatkiwa kuhudumia mjamzito mmoja lakini kutoka na wingi wao mmoja anahudumia wanne.

Alisema kutokana na hali hiyo mama wajawazito wanakosa staha na kuiomba serikali kuongeza wafanyakazi na maslahi kwa kuwa wapo wanne wakifanyakazi ya watu 12.

# SIKU YA UHURU WA VYOMBO VYA HABARI



Rais Samia Suluhu Hassan (kushoto), akimsikiliza Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN), Salome Kitomari, alipotembelea banda lao katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, Mei 3, mwaka huu, ambayo kwa Afrika yaliadhimishwa jijini Arusha. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU**





Baadhi ya wadau wa habari wakimsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) alipohutubia kwenye maadhimisho hayo.




Mwenyekiti wa MISA Tanzania, Salome Kitomari, akitoa ujumbe wa taasisi hiyo yenye matawi katika nchi za SADC, katika maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari, ambayo kwa Afrika yaliadhimishwa Mei 3, jijini Arusha, ikiwa ni mara ya kwanza kufanyika Afrika Mashariki.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (kushoto), akipata maelezo ya shughuli zinazofanywa na MISA Tanzania, kwa mwenyekiti wake, Salome Kitomari.

## HABARI KIMATAIFA



Viongozi wa nchi tajiri duniani G7; Marekani, Ujerumani, Italia, Ufaransa, Canada na Japan wakiwa pamoja kabla ya kikao chao jana. **PICHA: DW**

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# Russia yaongeza mashambulizi wakati G7 wakikutana kujadili vita

**LONDON,** Uingereza

KIONGOZI wa nchi tajiri duniani G7 wamefanya mkutano jana kujadili vita inayoendelea nchini Ukraine, huku mataifa yao yakiendelea kuahidi msaada zaidi wa kijeshi.

Katika mkutano huo Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelenskiy, amealikwa kushiriki.

Uingereza tayari iliahidi katika mkutano huo itatoa msaada wa kijeshi wa nyongeza wa dola bilioni 1.6 kwa Ukraine.

Waziri Mkuu wa Uingereza, Boris Johnson (pichani chini), alisema kuwa miongoni mwa viongozi wanaotoa msaada mkubwa wa kuiunga mkono Ukraine kijeshi ili kulisaidia taifa hilo kuvikabili vikosi vya Urusi tangu Rais Vladimir Putin aamuru kuivamia nchi hiyo.

Mpaka sasa serikali ya Uingereza imeshatuma makombora ya kuharibu vifaru, mifumo ya ulinzi wa anga na silaha nyingine nzito kuisaidia Ukraine.

Ahadi mpya ya msaada iliyotolewa kabla ya mkutano wa G7 inaongeza karibu maradufu fedha iliyotolewa na Uingereza kuisaidia nchi hiyo.

Serikali ya Uingereza ilisema kitita hicho cha fedha ni kikubwa kinaakisi matumizi makubwa kwa nchi hiyo kwenye mzozo tangu vita vya Iraq na Afghanistan.

"Hujuma ya kikatili ya Putin siyo tu inasababisha madhara yasiyoelezeka nchini Ukraine, bali inaitishia pia amani na usalama kote barani Ulaya," ilisema taarifa ya Johnson.

Waziri Mkuu Johnson alitoa kauli hiyo alipokuwa akilihutubia bunge la Ukraine.



Wiki iliyopita kiongozi huyo alikuwa wa kwanza kutoka mataifa ya magharibi kulihutubia bunge la Ukraine tangu kutokea kwa uvamizi wa Russia.

Jana, Johnson alitarajiwa kujiunga na viongozi wengine wa G7 kutoka mataifa ya Marekani, Ujerumani, Italia, Ufaransa, Canada na Japan katika mkutano huo kwa njia ya mtandao kujadili mzozo huo.

Mkutano huo unafanyika siku moja kabla Russia kuadhimisha Siku ya Ushindi hapo tarehe 9 Mei kukumbuka kumalizika kwa vita vikuu vya pili vya dunia barani Ulaya.

Uingereza ilisema msaada wa ziada inaotoa kwa Ukraine kutoka kwenye mfuko wa akiba unaotumiwa na serikali wakati wa dharura.

Kadhalika serikali ya Uingereza ilisema Johnson atakuwa mwenyeji wa mkutano wa wazalishaji wakubwa wa silaha baadaye mwezi huu kujadili kuongeza uzalishaji kutokana na kuongezeka kwa mahitaji yanayotokana na vita nchini Ukraine.

### RUSSIA YAENDELEA KUSHAMBULIA MIJI

Katika hatua nyingine Russia imeendeleza mashambulizi yake ikiyalenga maeneo kadhaa ndani ya Ukraine.

Vikosi vyake vilifyatua makombora mazito yaliyoulenga mji wa kusini wa Odesa pamoja na mji inaouzingira wa Mariopul ikitumai kuidhibiti bandari ya mji huo kabla ya maadhimisho ya Siku ya Ushindi hapo Jumatatu.

Ukraine ilisema wanawake, watoto na wazee wote waliokwama kwenye mji huo tayari wameondolewa kutoka kiwanda cha chuma walimokuwa wamejificha.

Hata hivyo kundi la wanajeshi bado limesalia kwenye eneo hilo na kiongozi wake Serhiy Volinski ametoa wito wa kupatiwa msaada wa kuondoka salama saa kadhaa baada ya raia wa mwisho kuondoka Azovstal.

Rais Zelenskyy aliahidi kutakuwa na mazungumzo ya kuwawezesha wanajeshi waliokwama nao pia kuondoka ingawa Russia haijaashiria uwezekano wa kuunga mkono suala hilo.

### 60 WAHOFIWA KUUAWA NDANI YA SHULE

Watu 60 wanahofiwa kufariki dunia baada ya shule moja mashariki mwa Ukraine, kushambuliwa na bomu.

Eneo ambalo lililotokea shambulio kuna mapigano makali huku vikosi vya serikali vinapambana na wanajeshi wa Russia na watu wanaotaka kujitenga.

Gavana wa Mkoa wa Luhansk, Serhiy Gaidai, alithibitisha vifo vya watu wawili, akisema watu 60 wanahofiwa kufa kwa kufunikwa chini ya vifusi vya shule huko Bilohorivka.

Takriban watu 90 walikuwa wamejihifadhi katika jengo hilo ambapo 30 waliokolewa, saba kati yao wakiwa wamejeruhiwa, aliongeza.

Gaidai alisema kuwa ndege ya Russia ndiyo iliyoshambuliwa majengo ya shule hiyo kwa bomu siku ya Jumamosi.

Madai yake hayakuweza kuthibitishwa kutokana na kutokuwapo kwa majibu ya haraka kutoka kwa Russia.

Luhansk imeshuhudia mapigano makali huku wanajeshi wa Russia na wapiganaji wanaotaka kujitenga wakijaribu kuzingira vikosi vya serikali, zaidi ya miezi miwili tangu kuanza kwa uvamizi.

Umoja wa Mataifa umerekodi vifo vya raia 2,345 na wengine 2,919 kujeruhiwa nchini humo na zaidi ya watu milioni 12 wakiikimbia nchi hiyo kuhofia usalama wao. **DW**

## Spika wa Bunge afariki dunia

**ABIDJAN,** Ivory Coast

SPIKA wa Bunge la Ivory Coast, Amadou Soumahoro, amefariki dunia akiwa na umri wa miaka 68, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Rais Alassane Ouattara.

Soumahoro aliyefariki Jumamosi alikuwa mwanasiasa wa Ivory Coast na mfuasi mwaminifu wa Rais wa Ouattara. Alikuwa mwanachama mwanzilishi wa Rassemblement des Républicains (RDR), chama cha kihistoria cha Ouattara, mwaka wa 1994.

Waziri wa zamani wa biashara wa Ivory Coast, Amadou Soumahoro, alikuwa spika ama rais wa Bunge la Kitaifa mwaka wa 2019, akichukua nafasi ya Waziri Mkuu wa zamani na kiongozi wa waasi Guillaume Soro.

Masuala ya kiafya yalimfanya awe nje ya nchi kwa muda mrefu katika miezi ya hivi karibuni. Mwaka jana, nafasi yake ilijazwa kwa muda na mmoja wa Makamu wa Rais wa Bunge la Kitaifa, Adama Bictogo.

## Wanajeshi 11 wauawa

**CAIRO,** Misri

WANAJESHI 11 wa Misri wameuawa na wengine watano kujeruhiwa walipokuwa wakikabiliana katika shambulio la kigaidi katika eneo la mfereji wa Suez.

Taarifa ya jeshi la nchi hiyo ilisema tukio hilo lilitokea katika eneo ambalo mfereji huo unaotokea katika rasi ya Sinai ambapo kuna ngome ya shughuli za kigaidi.

Jeshi limesema wanajeshi wengine watano wamejeruhiwa wakati wakijaribu kuudhibiti moto katika kingo za mfereji huo na kuongeza kwamba vikosi vya usalama vinaendelea kuwafuatilia na kuwazingira magaidi katika eneo hilo la Sinai.

Rais Abdel Fattah al-Sisil alisema operesheni hizo za kigaidi hazitashinda juhudi za nchi hiyo kuushinda ugaidi. BBC

# AZAM YAIPONGEZA KMC, YENYEWE YAKIRI HALI TETE

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Azam FC, Abdihamid Moallin, amewapongeza wapinzani wao, KMC FC baada ya kuwapa upinzani mkubwa wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 2-1 kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Azam Complex, Chamazi nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam juzi.

**Hata hivyo, wakati Moallin akitoa pongezi hizo, Kocha Mkuu wa KMC FC, Thierry Hitimana, amekiri maji ya shingo na kwamba wanahitaji kufanya usajili mkubwa kwa msimu ujao wa ligi hiyo.**

Makocha hao waliyasema hayo juzi baada ya timu hizo kucheza mchezo wa ligi hiyo kutoa jasho vikali kabla ya Azam FC kuibuka na ushindi huo unaoifanya sasa kufikisha pointi 32 ikiwa nafasi ya tatu baada ya kushuka dimbani mara 22 msimu huu huku wapinzani wao, KMC wakiwa nafasi ya 11 na alama zao 24.

Moallin alisema mechi ilikuwa ngumu sana kwa sababu wao walihitaji pointi na KMC FC wakitafuta alama hizo na hatimaye kufaidika kwa wachezaji wake kufanya yale aliyowaelekeza mazoezini.

"Mechi ilikuwa ya ushindani tulifanikiwa kucheza katika kipindi cha kwanza na kupata bao la mapema, KMC FC walionyesha upinzani mkubwa na walicheza vizuri na kufanikiwa kufunga bao moja," alisema Moallin.

Alisema baada ya kupata pointi tatu sasa wanarudi kufanyia kazi mapungufu yao huku wakijiandaa na mchezo ujao wa ugenini dhidi ya Mbeya City.

Kwa upande wa Hitimana alisema mechi nyingi walizopoteza zimetokana na makosa yao ya safu ya ulinzi hasa kutokuwa imara tangu msimu huu kuanza.

Alisema mabao waliyofungwa na Azam FC ni mepesi sana na aina hiyo hiyo ambayo walifungwa katika michezo iliyopita kwa sababu ya madhaifu ya safu ulinzi.

"Tunafunga mabao mepesi sana, aina hiyo ya mabao tulifungwa katika mechi tulizopoteza hapo awali, hii inatokana na kuwapo kwa udhaifu katika safu ya ulinzi, nina imani kwa sasa tunaenda kupambana hivyo hivyo kuhakikisha tunabaki katika ligi," alisema na kuongeza;

"Msimu ujao tunatakiwa kufanya usajili mkubwa hasa kwa kuzingatia kuimarisha nafasi ya ulinzi hususan beki ya kati," alisema Hitimana.

Alisema kwa sasa makocha wa timu zilizoko chini ya msimamo wanacheza kwa presha kubwa kwa sababu ya kila mmoja anahitaji kujikwamua katika nafasi ya kushuka daraja kulingana na uwiano wa pointi walizopishana kuwa mdogo.

## Minziro aiota 3 - bora Geita Gold

**NNa Dennis Fussi**

KOCHA Mkuu wa Geita Gold FC, Felix Minziro, amesema haoni wa kuizuia timu yake kumaliza tatu bora kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Minziro, ametoa kauli hiyo baada ya Geita Gold kuibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Kagera Sugar kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Kaitaba, Bukoba juzi Jumamosi na kutinga kwenye nne ya msimamo wa ligi hiyo. Minziro amesema ana uhakika timu hiyo itaendelea kufanya vizuri katika mechi zake zilizobaki na kwamba haoni wa kuizuia kumaliza kwenye tatu bora msimu huu.

"Tuna nafasi nzuri sana, naamini kabisa tunaweza kumaliza kwenye tatu bora, na nafasi hiyo naiona kwa uwazi kabisa," alisema Minziro mchezaji wa zamani wa Yanga.

Geita Gold sasa ipo nafasi ya nne ikiwa na pointi 31 ikipitwa alama moja tu na Azam waliopo nafasi ya tatu wakiwa na pointi 32 baada ya wote kushuka dimbani mara 22.

Geita Gold ambayo inashiriki Ligi Kuu ya Tanzania Bara kwa mara ya kwanza kwenye historia yake, ilipata bao hilo pekee na la ushindi kupitia kwa straika wao matata, George Mpole ambaye sasa amefikisha mabao la 12 na kuwa kinara wa kufumania nyavu sawa na nyota wa Yanga, Fiston Mayele.

Mwanzoni mwa msimu timu hiyo iliyokuwa inanolewa na Kocha, Etiene Ndayiragije ilikuwa na mwenendo mbaya kiasi cha kuhatarisha uwapo wao kwenye Ligi Kuu msimu ujao.

Uongozi wa wachimba madini hao waliamua kufanya mabadiliko ya benchi la ufundi pamoja na usajili wa wachezaji wenye uzoefu na ligi akiwamo beki, Kelvin Yondan na Juma Nyoso.

**LINAKUJA...**




Waziri wa Habari, Sanaa, Utamaduni na Michezo, Mohamed Mchengerwa, akipokea zawadi ya mpira kutoka kwa Meneja Mkuu wa Biashara wa Coca-Cola Tanzania, Hellen Masumba, wakati wa hafla ya uzinduzi rasmi wa ziara ya siku mbili ya Kombe la Dunia linalotarajiwa kuwasili nchini Mei 31, mwaka huu. Kulia ni Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini, Yusuph Singo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Absa yaipamba Dar City Marathon

**Na Jumanne Juma**

BENKI ya Absa Tanzania, imesema itaendelea kudhamini mbio zaidi nchini ili kudumisha utamaduni wa afya njema huku jana ikipamba Mbio za Dar City Marathon ziliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya mbio hizo, Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa benki hiyo, Aron Luhanga, alisema Absa imeridhishwa na namna mbio hizo zilivyoendeshwa na benki yao ikiwa na washiriki 45 kwa ujumla walioshiriki mbio za Km. 5, Km.10 na Km. 21.

"Kwetu sisi tunaamini katika wafanyakazi kuwa na afya ya mwili, lakini afya ya akili ili waweze kufanya kazi vizuri ndio maana tunajitahidi kushiriki katika mbio nyingi," alisema.

Luhanga alisisitiza kuwa mwakani pia watadhamini mbio hizo huku wakitarajia kuwa zitawavutia wadau wengi zaidi kushiriki.

## 'Wazazi, walimu mulikeni vipaji'

**Na Maulid Mmbaga**

DIWANI wa Kata ya Mbezi Juu, Anna Lukindo, ametoa wito kwa wazazi, walimu na wanafunzi kuwa na umoja na ushirikiano katika masuala mbalimbali yanayoleta maendeleo ikiwamo kuinua vipaji vya watoto na sekta ya elimu kwa ujumla.

Lukindo alitoa wito huo Dar es Salaam jana wakati akihutubia katika bonanza lililofanyika katika Shule ya Msingi Kilimani, likibebwa na kaulimbiu ya 'Michezo kwa Afya, Sensa kwa Maendeleo, Jiandae Kuhesabiwa'.

Alisema lengo kuu la bonanza hilo ni kuimarisha afya na kuchochea umoja baina ya wazazi, walimu na wanafunzi huku akiwapongeza walimu kwa jitihada wanazozifanya kuhakikisha kuwa watoto wanakuwa katika maadili mema wanapokuwa shuleni.

"Mmeona kuwa michezo ni afya ndiyo maana mkaandaa bonanza hili, nawapongeza na nafurahi kuona katika shule hii kunahamasishwa michezo, naamini pia vipaji mbalimbali tutaviona, na wale mtakaowaona kuwa wako katika nafasi nzuri kwenye mpira wa miguu na michezo mingine msisite kutuambia tusaidie kuendeleza vipaji vyao," alisema.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Francis Njoroge, alisema bonanza hilo wamekuwa wakiliandaa kila mwaka wakiwa na dhumuni la kuibua vipaji vya wanafunzi mbalimbali.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TIELEMANS ANUKIA ARSENAL

ARSENAL inakaribia kukamilisha uhamisho wa pauni milioni 40 kumsajili kiungo mbelgiji wa Leicester, Youri Tielemans, 25, lakini Real Madrid wako mguu sawa kumsajili nyota huyo kama 'Washikabunduki' hao watashindwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Sun)***

### RONALDO NA HATIMA

MSHAMBULIAJI Cristiano Ronaldo, 37, amezungumza na kocha wa zamani wa Manchester United, Sir Alex Ferguson kuhusu hatima yake klabuni hapo katika mfululizo wa vikao vyao vya siri. ***(Mirror)***

### JOHNSTONE KUTUA SPURS

TOTTENHAM Hotspur wanajiandaa kumsajili mlinda mlango wa West Brom na England, Sam Johnstone baada ya Manchester United kuamua kuachana na mpango wake wa kumsajili kipa huyo. ***(Mirror)***

### POGBA NA JUVENTUS

KIUNGO wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba amefanya mazungumzo na Juventus kuhusu kurejea Turin mwishoni mwa msimu. ***(Football Transfers)***

### ERIKSEN HAKIJAELEWEKA

KOCHA wa Brentford, Thomas Frank anataka hatima ya baadaye ya kiungo wa Denmark, Christian Eriksen, 30, iamuliwe kabla ya kumalizika kwa msimu huu. ***(Mail)***

### DIAZ ATAKIWA WEST HAM

KLABU ya West Ham inaongoza mbio za kumsajili mshambuliaji wa Blackburn na Chile, Ben Brereton, 23. ***(Sun)***

### UNITED WASHAURIWA KUSAJILI

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ralf Rangnick anatarajia kikosi hicho kitaongezewa nguvu kwa kuwasajili wachezaji wapya sita au nane msimu ujao pamoja na kuja kwa kocha mpya, Erik ten Hag. ***(Mirror)***

### TAGLIAFICO KUONDOKA AJAX

MLINZI wa Ajax na Argentina, Nicolas Tagliafico, 29, anajiandaa kuondoka kwenye klabu yake hiyo ya Uholanzi mwishoni mwa msimu huu, licha ya mkataba wake kubaki mwaka mmoja zaidi. ***(Fabrizio Romano on Twitter)***

### PHILLIPS ATULIZA AKILI

KIUNGO wa Leeds United na England, Kalvin Phillips, 26, amesema kwa sasa amejielekeza zaidi kumaliza msimu wa Ligi Kuu England akiwa na timu yake hiyo ya utotoni licha ya kuhusishwa na kuhamia Klabu za Aston Villa na Manchester United katika majira ya joto. ***(Manchester Evening News)***

### SAINT-MAXIMIN HAONDOKI

MLINZI wa Ufaransa, Allan Saint-Maximin, 25, amesema hajioni akiondoka Newcastle msimu huu. ***(Goal)***

### PAREDES AWAITA REAL MADRID

KIUNGO wa Paris St-Germain, Leandro Paredes amesema "ana ndoto" ya kuchezea Real Madrid. ***(TyC Sports on Twitter)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# KLOPP AANZA KUUKATIA TAMAA UBINGWA EPL

## Ninavyoona ni ngumu sana kwa Man City kuacha pointi katika kila mchezo uliopo mbele...

**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp haoni Manchester City ikiteleza katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England baada ya timu yake kudondosha pointi kwenye Uwanja wa Anfield kwa mara ya kwanza tangu Oktoba katika sare ya bao 1-1 dhidi ya Tottenham, Jumamosi.

**Matokeo hayo yanaifanya Liverpool kuwa kileleni mwa msimamo wa ligi kwa tofauti ya mabao, lakini vijana wa Pep Guardiola wanaweza kurudi katika uongozi kwa pointi tatu zikiwa zimesalia mechi tatu, kama jana Jumapili walifanikiwa kuwafunga Newcastle United.**

Son Heung-min aliwafungia Spurs dakika 56 kwa shambulizi la kushtukiza akicheza vizuri na Harry Kane, kabla ya Liverpool kusawazisha kupitia kwa Luis Diaz dakika 16 kabla ya mechi kumalizika.

Katika mchezo huo, Spurs walionekana kama wangeondoka na pointi zote tatu, kama washambuliaji wake wangekuwa makini, kwani walikosa nafasi kadhaa za wazi.

Mara baada ya mchezo huo Guardiola aliwaambia waandishi wa habari, kwa vyovyote hakuna uwezekano wa Man City kuteleza kwenye mbio hizo za ubingwa.

"Sioni," alisema Klopp alipoulizwa kama Man City wanaweza kupoteza pointi. "Natamani ningefikiria tofauti lakini sioni.

"Tatizo langu si kama City itaibomoa Newcastle. Ni Aston Villa siku ya Jumanne.

"Tuna pointi zaidi kuliko hapo awali kwa hiyo ni nzuri na ni bora zaidi kuliko tulipokuwa chini kwa bao 1-0. Bao hilo ni muhimu sana. Lakini si kile tulichotaka, lazima tukikabili na tutaweza," aliongeza.

"Ninavyoona ni ngumu sana kwa Man City kuacha pointi katika kila mchezo uliopo mbele yao kwa sasa, sisi tumeshindwa kutumia nafasi vizuri na sasa kazi kubwa iko mbele yetu."

Liverpool ilikuwa ikijipanga kutwaa mataji manne msimu huu, huku tayari mkononi ikiwa na Kombe la Carling.

Pia inawania kulibeba taji la FA na lile la Carabao, huku pia ikiwa imetinga fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya ambayo itakutana na Real Madrid mjini Paris baadaye mwezi huu.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
YOUNG AFRICANS
VERSUS
TANZANIA PRISONS
1 | 1.24
X | 4.79
2 | 11.73

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# Miaka 5 ya SportPesa y

**Na Frank Monyo**

KATIKA kipindi cha miaka mitano ya Kampuni ya SportPesa Tanzania kuwapo hapa nchini wamechangia pato la taifa kwa kulipa kodi kwa serikali kiasi cha Sh. bilioni 434.7 (majumuisho ya kodi zote), huku washindi waliopatikana kutokana na kubashiri kwa ufasaha wakiwa wamelipwa jumla ya Sh. bilioni 63.3, anaeleza Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni hiyo, Tarimba Abass, katika makala haya maalum.

Tarimba alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam, wakati akielezea mafanikio ya kampuni hiyo ndani ya miaka mitano tangu kuanza shughuli zake nchini Mei 09, 2017.

**Tarimba, alisema kuzaliwa kwa SportPesa ni baada ya kuona fursa ya kuwasaidia Watanzania kuwainua kiuchumi na kuipatia serikali mapato makubwa sambamba na kupata faida na kuwa tayari kushindana na washindani wengine kiweledi na si kijanjajanja ili Watanzania waweze kuiona kampuni hiyo kuwa ni bora na inafaa.**

"Uwapo wetu Tanzania uziondoa zile kodi nyingine za PAYE na vile vidogodogo, sisi tumeshailipa serikali shilingi bilioni 434.7, ni fedha nyingi, watu wasituone ni watu wa mchezo wa kubahatisha, wengine wanatutania wanatuita watu wa kamari, tunafanya mchango mkubwa pengine kuliko viwanda vingi na sidhani kama kuna mfanyabiashara anaweza kulipa fedha nyingi kama hizi," alisema Tarimba.

Aliongeza kuwa mpaka sasa kampuni hiyo imetoa zawadi za mbalimbali zenye thamani ya Sh. bilioni 344.4.

"Zawadi ambazo tumewalipa Watanzania tangu tumeanza Mei 2017 mpaka leo ni Sh. bilioni 344.4, hivyo naweza kusema tumetekeleza ile azma yetu, tutawasaidia Watanzania kuwainua kichumi na humu ndani tumeshatoa Jackpot mara sita zenye thamani tofauti tofauti.

"Kuna watu wamepata milioni 200 wengine 300, nyingine nakwenda mwenyewe nawaona, familia za watu masikini zinabadilika kuwa za uchumi wa kati na kuendelea kwa kufanyabiashara kwa kutumia fedha walizoshinda SportPesa," alisema.

Tarimba anasema kuwa zawadi kubwa ambayo SportPesa imewahi kuitoa ndani ya miaka mitano ni Sh. milioni 800 ambayo walishinda vijana wawili mmoja akifanya kazi Jeshi la Magereza na mwingine Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) ambao waligawana milioni 400 kila mmoja.

"Hawa watu naweza kusema kuwa wanajumuika na wengine waliopata milioni 20, 30 na milioni 40 hao ni wengi sana, hii tunakwenda kuwawezesha na wao pia wamelipa kodi serikalini kupitia zawadi wanazopata," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema SportPesa ni kampuni pekee kwa sasa ambayo inayo Jackpot ya Sh. bilioni 1.2 ipo inasubiri mtu kushinda. "Niambie Mtanzania akipata pesa kama hiyo umemtoa katika hatua gani, umempeleka hatua gani? Alihoji Tarimba.

Tarimba ambaye amewahi kuwa Mkurugenzi wa Bahati Nasibu ya Taifa enzi hizo, alisema kuwa 'betting' ni mchezo wa burudani, na mchezo wenye uelewa ndio maana unaitwa 'skill game' kwa kuwa ni mchezo ambao unachezwa na watu wenye uelewa na uzoefu.

"Hii si pata potea kwamba uchukue namba 1, 2, 3 useme kwamba mimi najaribu namba 3 hapana, wachezaji wote wa 'betting' hata kama watu wanawatania kwamba wanacheza watu wasio na kazi, naweza kusema ni uchache wa uelewa, hata wale wanaowasema wachezaji wa 'betting' kwamba wanajazana kwenye vibanda wanasahau faida wanazozileta kwenye nchi hii kwa kulipa kodi," alisema Tarimba na kuongeza kuwa;

"Mojawapo ya faida ni kodi zinazolipwa, uwapo wa hawa watu kwenye vibanda ambavyo vimesajiliwa, na wakacheza wanachangia vilivyo pato la taifa, hiyo nazungumzia tu SportPesa kwa miaka mitano, je, kwa makampuni mengine katika kipindi cha miaka mitano, tumeingiza kiasi gani?" Alihoji Tarimba.

Alisisitiza kuwa anatamani siku moja kufanyike mdahalo kuhusiana na michezo ya 'betting' ili watu waone



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya Sport Pesa Tanzania, T katika ofisi za kampuni hiyo jijini Dar es Salaam kuelezea mafanikio yaliopat
**PICHA: SPORT PESA**

CHEZA USHINDE KASINO




# alipa kodi bilioni 434/-



arimba Abass, akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki
ikana ndani ya miaka mitano tangu kuanzishwa kwa kampuni hiyo nchini.

> Kinachowapeleka kucheza kwenye kampuni za nje ni kwa sababu hawalipi kodi, serikali ikashauriwa embu punguzeni hapo ili kuona itasaidia watu kucheza zaidi Tanzania.

na kufunguka macho, kwamba michezo ya kubahatisha hasa 'betting' ni michezo yenye faida kubwa kwa taifa hili.

Tarimba ambaye ni Mbunge wa Kinondoni, alisema kuwa kwa mfano kwa mwaka 2021 kodi ya wanaocheza na kupata zawadi walikuwa wanalipa asilimia 20 serikalini, akipata milioni 100, milioni 20 inakwenda serikalini.

Alifafanua kuwa "serikali ilipunguza asilimia tano, sasa kupunguza kwake ilikuwa ni nini, kwamba kuna watu sasa hivi wanacheza 'betting' kwenye kampuni za nje ambazo hazilipi kodi nchini, taifa halipati faida.

"Kinachowapeleka kucheza kwenye kampuni za nje ni kwa sababu hawalipi kodi, serikali ikashauriwa embu punguzeni hapo ili kuona itasaidia watu kucheza zaidi Tanzania.

"Hatima yake ilivyoondolewa asilimia tano na sasa watu wakawa wanalipa asilimia 15, ikaongeza thamani ya watu wanaocheza na fedha ambazo zimekuja serikalini kutoka Julai 2020 hadi Desemba ilikuwa bilioni 10.6 baada ya mabadiliko serikali kuondoa asilimia tano mwaka 2021 serikali imepata kodi bilioni 14."

Alisema kumbe kwenye nchi kama ukipunguza kodi, unachochea matumizi zaidi na hivyo unasababisha serikali ipate zaidi, na kwamba watu walikuwa na hofu endapo serikali ikipunguza itapata hasara jambo ambalo si la kweli.

Tarimba ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Kinondoni, alisema katika kipindi cha miezi sita wachezaji walilipa kodi ya Sh. bilioni 27 inayotokana na zawadi, jambo ambalo linaonyesha michezo hii kama itakuwa inasikilizwa vizuri na wafanya inaweza kusaidia kuinua pato la taifa.

"Katika mwaka 2021-2022 serikali ilikuwa imepanga ipate bilioni 150 kwenye mwaka wa fedha ambao unamalizika keshokutwa, hivi ninavyozungumza makusanyo yapo asilimia 90 na zaidi, hivyo serikali inakwenda kufikia malengo yake," alisema Tarimba.

Akizungumzia mipango ya kampuni hiyo kwa miaka mitano ijayo, Tarimba alisema ni kuhakikisha mafanikio ambayo yamepatikana tangu kuanzishwa SportPesa yanaongezeka na kuwa kampuni inayoongoza kama ilivyo sasa kwenye kampuni za kubashari.

"Hatuna sababu ya kukaa nyuma, kwa sababu tuna weledi wa kutosha, kwa mfano wafanyakazi wetu nikiwamo mimi pia tunauzoefu mkubwa sana katika uendeshaji wa michezo hii si biashara, masuala ya kisheria, masuala ya kimifumo na teknolojia... tunauzoefu mkubwa sana, kibiashara tunavyokubalika sasa tungependa kuona tuwe maradufu," alisema na kuongeza kuwa;

"Sisi madhumuni yetu ni kutanuka kutoka asilimia 30 ya 'marketing share' na kufikia asilimia 40 hadi 50 na hiyo ina hakisi kwamba tungependa kukubalika na Watanzania, yaani mtu akifikiria kubetting Tanzania aifikirie SportPesa," alisema.

Aidha, alisema kampuni hiyo imeajiri Watanzania zaidi ya 104, na katika miaka mitano ijayo wanatarajia kuongeza zaidi ajira pamoja na kuongeza thamani ya zawadi kwa wachezaji.

"Kwa mfano hii bilioni 1.2 ya Jackpot ikishaliwa, tunampango wa kuitambulisha Jackpot nyingine yaani tuwe nazo mbili. Ikumbukwe kuwa Jackpot hii ilianza kwa Sh. milioni 200, lakini imewekezwa hadi kufika bilioni 1.2 sasa tunataka kuja na Jackpot mpya baada ya hii kuliwa, tunampango kuwa na Jackpot ya milioni 200, pia tuna Jackpot ambayo itaanza kwenye bilioni 1 hii ndio muelekeo wetu wa kutoa zawadi zaidi na kuwafanya Watanzania kupata fedha zaidi kutoka katika shughuli zetu," alisema Tarimba.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU,
BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 09/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2787 | Wazito vs Nairobi City Stars FC | 3.50 | 2.90 | 2.28 |
| 15:00 | 3382 | Fiorentina Youth vs Sampdoria Youth | 2.04 | 3.60 | 3.01 |
| 15:15 | 5585 | Selangor Pkns vs Kelantan United FC | 2.34 | 3.27 | 2.73 |
| 16:00 | 4615 | Teplice B vs Mlada Boleslav B | 2.33 | 3.36 | 2.68 |
| 16:30 | 4985 | FK Sumgayit vs Keshla FK | 2.54 | 2.83 | 2.83 |
| 17:00 | 3413 | Torino Youth vs Atalanta Youth | 3.10 | 3.80 | 2.07 |
| 17:00 | 3996 | Eastern Company SC vs Arab Contractors | 3.64 | 2.90 | 2.20 |
| 17:30 | 1462 | Neroca FC vs Churchill Brothers | 3.40 | 3.45 | 1.94 |
| 17:30 | 3524 | Petrolul Ploiesti vs Concordia Chiajna | 1.51 | 3.60 | 6.24 |
| 18:30 | 3213 | Klubi 04 vs Salpa Salo | 1.59 | 4.57 | 3.99 |
| 18:30 | 4136 | TPS Turku vs Pif Jalkapallo | 1.18 | 6.04 | 11.68 |
| 18:45 | 5956 | Gabala vs Neftchi Baku | 3.51 | 3.12 | 2.02 |
| 18:55 | 4655 | AL Nahdha vs Alshoulla | 2.85 | 2.85 | 2.75 |
| 18:55 | 4694 | AL Jeel vs AL Ain | 2.68 | 2.78 | 2.73 |
| 19:00 | 1397 | Raufoss vs Bryne | 1.88 | 3.49 | 3.54 |
| 19:00 | 1538 | Young Africans vs Tanzania Prisons | 1.24 | 4.79 | 11.73 |
| 19:00 | 1560 | Doxa Katokopia vs Ethnikos Achnas | 2.42 | 3.26 | 2.86 |
| 19:00 | 1843 | Ranheim vs Stabaek | 2.82 | 3.35 | 2.24 |
| 19:00 | 3761 | Sandnes Ulf vs Fredrikstad | 2.31 | 3.40 | 2.67 |
| 19:00 | 4174 | Gornik Leczna vs Nieciecza KS | 2.40 | 3.31 | 2.63 |
| 19:00 | 4783 | Anorthosis Famagusta vs Pafos FC | 2.01 | 3.30 | 3.70 |
| 19:00 | 4908 | KuPS Akatemia vs Jippo | 2.69 | 3.91 | 2.12 |
| 19:00 | 5223 | Kfum Oslo vs Brann | 3.40 | 3.50 | 1.92 |
| 19:00 | 5328 | Zaglebie Sosnowiec vs Sandecja | 2.36 | 3.06 | 2.86 |
| 19:00 | 5748 | Sogndal vs Kongsvinger IL | 1.72 | 3.66 | 4.10 |
| 19:30 | 3320 | Farco FC vs Coca Cola | 4.07 | 2.88 | 2.07 |
| 20:00 | 1312 | IFK Varnamo vs BK Hacken | 3.26 | 3.35 | 2.02 |
| 20:00 | 1648 | Viborg FF vs Vejle BK | 1.68 | 3.70 | 4.79 |
| 20:00 | 1942 | Helsingborg vs Norrkoping | 3.50 | 3.36 | 1.94 |
| 20:00 | 2114 | Orebro SK vs Ostersunds | 1.80 | 3.74 | 4.24 |
| 20:00 | 3517 | Antalyaspor vs Konyaspor | 2.58 | 3.33 | 2.58 |
| 20:00 | 3714 | GIF Sundsvall vs Degerfors | 2.19 | 3.40 | 2.87 |
| 20:00 | 5249 | Skovde Aik vs Halmstads BK | 3.69 | 3.49 | 1.99 |
| 20:00 | 5508 | Hapoel Haifa vs FC Ashdod | 2.54 | 3.27 | 2.49 |
| 20:10 | 4428 | Elfsborg vs Djurgardens IF | 1.95 | 3.50 | 3.31 |
| 20:30 | 1336 | Rapid Bucuresti vs U Craiova SA | 2.09 | 2.97 | 3.77 |
| 20:30 | 4341 | FC Trollhattan vs Qviding Fif | 1.68 | 3.75 | 4.18 |
| 21:00 | 2655 | De Graafschap vs FC Eindhoven | 2.07 | 3.43 | 3.28 |
| 21:00 | 4344 | Diosgyori Vtk vs Soroksar | 1.57 | 3.74 | 5.05 |
| 21:15 | 2555 | FC Wil vs FC Winterthur | 2.82 | 3.70 | 2.10 |
| 21:15 | 3253 | FC Aarau vs FC Stade LS Ouchy | 1.53 | 4.27 | 4.66 |
| 21:45 | 1474 | Fiorentina vs Roma | 2.30 | 3.28 | 2.93 |
| 21:45 | 3402 | Derry City vs St Patricks | 1.82 | 3.41 | 3.89 |
| 21:45 | 3430 | Shamrock Rovers vs Sligo Rovers | 1.36 | 4.18 | 7.97 |
| 21:45 | 5034 | Sheffield Wed vs Sunderland | 1.98 | 3.32 | 3.66 |
| 22:00 | 1983 | Cobresal vs Everton Vina del Mar | 1.96 | 3.16 | 3.65 |
| 22:00 | 2833 | Girona vs Tenerife | 2.20 | 3.17 | 3.22 |
| 22:00 | 4162 | Talaea El Gaish vs National Bank | 2.32 | 2.83 | 3.43 |
| 22:15 | 4986 | Belenenses vs Famalicao | 2.83 | 3.13 | 2.48 |
| 23:30 | 2501 | Univ San Martin vs Alianza Lima | 5.81 | 3.82 | 1.50 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Mei 9, 2022
Nipashe



Miaka 5 SportPesa yalipa kodi bil. 434/-

UKURASA 22

ACHENI WAJE...



Wachezaji wa Yanga, mshambuliaji Fiston Mayele (kulia) na beki Shabani Djuma wakipasha katika moja ya mechi za Ligi Kuu msimu huu. Nyota hao wataiongoza Yanga katika mechi ya ligi hiyo dhidi ya Tanzania Prisons itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa leo. **PICHA: MAKTABA**

# NABI ATAMBA KURUDI NA USHINDI YANGA SC

## Asema kukosekana kwake chanzo sare mbili, Prisons nao...

**Na Saada Akida**

NI pointi tatu tu leo! Hiyo ni kauli ya Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu Bara utakaopigwa leo saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Yanga ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 56, 13 mbele ya Simba iliyoko nafasi ya pili, tofauti ya alama hizo zikiwa ni kabla ya mechi yao ya jana usiku dhidi ya Ruvu Shooting.**

Nabi alisema baada ya kushindwa kupata matokeo mazuri ya ushindi dhidi ya Ruvu Shooting katika mchezo uliopita, sasa wanaingia katika mechi hiyo dhidi ya Tanzania Prisons kutafuta ushindi.

Alisema lazima leo watapambana kutafuta ushindi kutokana na jinsi morali ya wachezaji wake ilivyo juu baada ya kutopata matokeo mazuri katika michezo miwili iliyopita.

"Tunahitaji kupata ushindi katika mchezo wa kesho (leo), tunatambua itakuwa mechi ya ushindani mkubwa kulingana na nafasi waliyopo wapinzani wetu," alisema Nabi akiihofia Prisons ambayo ipo nafasi ya pili kutoka mkiani ikiwa na alama 22 sawa na wastani wa pointi moja katika kila mchezo kati ya 22 iliyocheza hadi sasa.

Kuhusu Fiston Mayele, kuwa na presha ya kufunga kwa sababu wapo sawa idadi ya mabao na Gerge Mpole wa Geita Gold FC, alisema wachezaji wake wanachowaza ni matokeo ya timu na si mbio za kufunga.

"Mayele hachezi pekee yake, asipofunga basi kuna mchezaji atafunga kwa ajili ya kusaidia timu kupata pointi tatu muhimu katika mchezo wetu dhidi ya Tanzania Prisons," alisema na kuongeza;

"Tanzania Prisons si timu ya kuibeza kwa sababu wako chini bali tunaenda kucheza kwa umakini mkubwa kwa sababu timu zinazoshika nafasi ya chini zinakuwa na ugumu mkubwa na kutaka kupambana kutafuta matokeo kwa timu kubwa,"alisema Nabi.

Alisema matokeo ya michezo miwili iliyopita yalitokana na kutokuwapo katika benchi akitumikia adhabu ya kadi nyekundu aliyopewa katika mchezo wa robo fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam dhidi ya Geita Gold FC.

"Tangu nimeanza ukocha sijawahi kupewa kadi nyekundu, ninashangaa kuona taarifa kwamba nimetukana uwanjani, jambo ambalo linaniumiza kwani kutokuwapo benchi imekuwa sababu ya kutopata ushindi katika michezo miwili, lakini nimerejea na lazima kupata ushindi katika mchezo wa kesho (leo)," alisema Nabi.

Kocha Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shaban Ally alisema wanaingia na mbinu nyingine katika mchezo huo tofauti na michezo iliyopita ili kuhakikisha wanapata pointi.

Alisema wanatambua wanaenda kucheza na timu ambayo haijapoteza mechi, lakini hilo halitawafanya kuwaogopa na zaidi watashuka dimbani kwa nidhamu ya hali ya juu kutafuta matokeo.

"Tumejiandaa vizuri mbinu tulizoingia nazo katika michezo iliyopita zitakuwa tofauti kabisa na mchezo wa kesho kwa sababu tunahitaji kupata matokeo ili kujinasua katika kushuka daraja," alisema Kocha huyo msaidizi.

Nahodha Benjamini Asukile alisema wamejiandaa vizuri na kila mmoja wao anafikiria mechi hiyo ya leo kwa sababu kwao wanaingia wanauchukulia kama fainali ya kutafuta pointi muhimu ya kujinasua katika nafasi ya chini ya msimamo.

# Sakho azua vita Al Ahly, Orlando

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa soka Afrika, Al Ahly na Orlando Pirates ni kati ya timu zinazotajwa kumuwinda kiungo mshambuliaji wa Simba raia wa Senegal, Pape Sakho.

Klabu ya Simba imethibitisha kuwindwa kwa mchezaji huyo, ingawa imesema bado ana mkataba mrefu na klabu hiyo, lakini ikaongeza kuwa hakuna mchezaji asiyeuzwa duniani.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally amesema siyo timu hizo tu, bali mchezaji huyo amekuwa akiulizi-wa na klabu mbalimbali Afrika na nje ya bara hili kwa ajili ya kupata huduma yake.

"Ingekuwa ni ajabu sana kama Sakho mkapa sasa asihusishwe na klabu yoyote ile, na sisi kama Simba tungekuwa tumefeli. Siyo Al Ahly tu, hata Orlando nayo inemuulizia, kwa sababu kiwango alichonacho hakuna klabu yoyote yenye kutaka mafanikio isitamani kuwa naye, kwa hiyo watu wasishangae kusikia anauziliwa, ni kwa sababu ana ubora," alisema Ahmed.



Alisema kuwa msimamo wa Simba ni kwamba wasingependa kuwa wanauza wachezaji wao, ila wakati mwingine huwa zinakuja ofa nono ambazo huwa zinaitingisha klabu na mchezaji mwenyewe.

"Kama itakuja ofa nzuri vya kutosha, tukaona tukimwachia tunaweza kupata Sakho mwingine kwa bei zuri, tutafanya hivyo, wakati tunamuuza Miquissone (Luis) watu hawakujua kama atapatikana mbadala mwingine wa kufanya vizuri, akaja Sakho. Mpira ni biashara, unauza na kununua, na hakuna mchezaji duniani asiyeuzwa, maulizo ya mchezaji huyu yako mengi, lakini ikumbukwe kuwa bado ana mkataba na Simba," alisema.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >